# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

Verbatim Report Of

## DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL

## KINANGO CONSTITUENCY, HELD AT KINANGO SECONDARY SCHOOL

ON

# 15TH OCTOBER 2002

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL , KINANGO CONSTITUENCY, HELD AT KINANGO SECONDARY SCHOOL ON 15TH OCTOBER 2002**

**Commissioners Present:**

1. Mohammed Swazuri Commissioner

**Secretariat Staff:**

1. Noor Awadh - Assistant Programme Officer
2. Lydia Moraa - Verbatim recorder
3. Mwero Mkala - District Coordinator

The meeting started with a prayer from Rev. John P. Katana at 11.21 a.m.

**Mwero Mkala**: Wandugu wananchi wa Kingango hamjambo?

**Chorus:** Hatujambo.

**Mwero:** Tumewangojea wengine lakini tumeona tafadhali tuanze watatupata tukiwa

tunaendelea. Na kabla kuendelea na mambo yetu wa leo, ningeomba mzee moja ajitolee ama mama moja atufungulie makao huu kwa maombi tafadhali; Reverend.

**Rev. John P. Katana**: Baba yetu ulie juu mbinguni, tunatoa shukurani mbele yako asubuhi ya leo, kwa ajili wa ulinzi wako, umetupenda, na sisi e Mfalme tuko mahali hapa, Mungu wa majeshi kwa ajili ya kuangalia mambo haya ya Katiba, tunakushukuru kwa sababu kila jambo lililoanza limeanza vyema, na hata kwa wakati huu e mfalme kila jambo litakwenda kutendeka sawa sawa. Uwasaidie wenzetu hawajafika, na tunashukuru Bwana hata kwa ajili- vya viongozi ambao wako mbele zetu, Tume ya Marekebisho hii ya Katiba ambao wameweza kufika, tunaomba Bwana utuwezeshe ili kila hatua

ambayo tutaenda kuichukua Bwana ikaweze kuwa vile ambayo umetaka tukaweze kufanya kwa ajili ya nchi yetu, kwa yesu Kristo Bwana na Mwokozi wetu. Amen.

**Mwero**: Kabla ya kuendelea nilikuwa ninaulizwa hapo nje Commissioner Swazuri ni gani, kwa hivyo nita chukua dakika moja kuwajulisha wale wageni ambao wametoka Nairobi, halafu tuendelee na ratiba yetu. Huyu dada ambaye ameshika kipaza sauti ama kinasa sauti anaitwa Moraa, na yule ambaye amekaa mkono wa kiume anaeandika hapa anaitwa Bi. Noor, na huyu ambaye anaandika ni Commissioner wetu mtoto wa Kwale, ni mwalimu wa Chuo Kikuu cha Nairobi anaitwa Daktari Mohammed Swazuri, anatoka hapa Waa. Kwa hivyo ambapo wanauliza Swazuri ni yupi, ndio huyu hapa. Yeye ni mmoja wa wale Commissiners 29 wa Tume ya Marekebisho ya Katiba katika nchi yetu ya Kenya. Kwa hayo machache na mengi nina mkaribisha Mwalimu Swazuri, akaweze kuanzisha kikao hiki rasmi na kuendeleza. Karibu Bwana Swazuri.

**Com. Swazuri:** Asante sana Bwana District Coordinator, sisi tumekuja hapa kwa ahadi tulioweka mwezi wa nne, tulikuwa hapa tarehe 30 mwezi wa nne, tukasema kwamba tutaenda Kenya yote tukusanye maoni tumalize turudi hapa. Tumeshaandika report turudi hapa ili muuje mpate nafasi ya kuangalia kama yale mliosema yametekelezwa au la. Tuwapatie nafasi ili muweze kujadili, kutoa maoni zaidi kuisifu au kuikashifu hio report tuliotoa, kuongeza au kupunguza vile mnavyo taka, ndio maana tumekuja hapa. Kwa hivyo tukimaliza hapa, tutakuwa na kongamano au mkutano wa wajumbe ambao mumewachagua, na wale wa Bunge tofauti tofauti ambayo yatakutana Nairobi kuanzia tarehe 28, kwa mwezi mmoja nao pia watakuwa na nafasi ya kuiangalia report hii. Ile ambayo itasahihiswa baada ya maoni yenu ili nao wazidi kuichangia mpaka wakubaliane iwe sasa ni Katiba ya Kenya wapeleke bunge ipitishwe. Kwa hivyo hiyo ndiyo sababu ambao imetuleta hapa. Lakini tunasikitika watu ni kidogo sijui ni kwa sababu ya mvua au sababu gani, lakini watu ni kidogo. Lakini kwa sababu muda unaenda, wale wale tulio nao ndio tutaendelea nao.

Kwanza tutaanza na sura ya ile Katiba yenyewe. Tutaanza na lugha, wananchi walilalamika lugha ya Katiba ya ki-sheria ni ngumu, sasa tumeandika kwa kiingereza au Kiswahili ambacho ni kile chembamba, ambacho chaeleweka kwa mwananchi wa kawaida. Ukiangalia mtakuta report zimetolewa kwa Kiingereza na kwa Kiswahili. Draft, huu mswada bado hayatolewa kwa Kiswahili, bado kuna watu wanatafsiri, lakini hata ikitoka huu mswada utakuwa lugha yake sio ngumu, kama vile ambavyo watu wengine wanatumia, ili kila mtu waweze kuelewa.

Halafu, Katiba yetu ambao tunapendekeza sio ndefu sana walakini sio fupi sana. Sio ndefu sana ikawa inalemea, wala sio fupi sana ikawa ni kitu inaweza kutupa. Tumefanya hivyo, kwa sababu tumefanya marekebisho mara mbili, tuna vitu ambavyo tumeviona lazima viingie kwenye Katiba vile vya muhimu kabisa tumeviweka kwenye Katiba. Kuna vitu ambavyo nisheria lazima zirekebishwe, hivyo hatukuviandika kwenye Katiba. Tutaandika orodha mbali halafu tutapelekea zile sheria ambazo zina husika au wale wanahusisha Wa-Bunge ili warekebishe sheria hizo. Kwa hivyo kuno mambo mengi ambayo pengine mumeyasema tumeyachukulia maanane lakini hamtayaona kwenye Katiba, tutapeleka tu kwenye zile sheria zinazo

husika. Halafu ninataka kuzungmuzia mambo ambayo yako tofauti baina ya ile Katiba ya sas na hii Katiba ambao tumependekeza. Tusema haya ni mambo ambayo ni mapya ambayo wananchi wengi walitaka ambayo tumejaribu kuyaweka katika Katiba hii mpya. Neno la kwanza ni kwamba Katiba hii imetengenezwa na wananchi. Sio Katiba ya watu kidogo, ni wananchi wote walihusika, either kutoa maoni au kusikiliza kutoa maoni, au kuhudhuria mikutano au kwenda kusikiliza civic education. Kwa hivyo ni kwa ufupi ni mambo ambayo yamezungumzwa na yamekubaliwa na wananchi wote.

Jambo la pili ni kwamba Katiba ya sasa hii tunapendekeza tunatilia mkazo zaidi uhuru wa mwananchi wa Kenya, uhuru na kutekeleza maisha yao wananchi wa Kenya ndio unatiliwa mkazo. Nilikuwa ninasema maswala ya wananchi ndiyo yametiliwa mkazo, uhuru wa wananchi ndiyo yametiliwa mkazo, mapendekezo ya wananchi ni kwamba tumeisikilza sana maoni ya wananchi. Pili tumesema kwamba tunaondoa ubaguzi wa aina yoyote katika taifa la Kenya. Sheria zitakuwa zinaangalia wananchi wote' weusi' wekundi, warefu wafupi wakutoka wapi, wadini gani, wamila gani, sheria yote iko sawa kwa wananchi wote. Hilo ni jambo ni tofauti kubwa sana, mwananchi wa kawaida sasa amepewa haki nyingi za kimsingi, haki ya elimu, haki ya afia, haki ya kuzungumza, haki ya matembezi, haki ya kuishi mahali anapotaka, na pia tumeandika ni nani atatekeleza haki hizo. Tumeandika na zita lindwa na nani.

Jambo jingine nikwamba sasa tumeharamisha hongo, corruption, sasa ni kinyume cha sheria mtu yoyote kuhusika katika shughuli za hongo. Kama ni askari, kam ni mtu wa kawaida, kama ni wakili, kama ni jaji, mambo ya hongo kama ni viongozi yote yameondolewa.

Upande wa uchaguzi, kuna mambo mapya mengi pale, kwanza tumesema kura zitakuwa sikuandikishwa kila siku. Kuanzia tarehe moja January mpaka tarehe 31 December. Kila mwaka hata kama sio mwaka wa kura, mtu yeyote akifika miaka 18, akipata kitambulisho yataenda kuchukua kitambulisho cha kura. Hiyo ni tofauti kubwa. Pia tukasema kura zitakuwa zikipigwa kwenye madebe yanaoneka wazi, transparent, si madebe meusi, na tukasema kura zitahesabiwa kwenye kituo pale pale tujue mshindi ni nani katika kila kituo. Tukasema wakichaguliwa wabunge na kama hawafanyi kazi zao, au ma-councillor, kiongozi yoyote akichaguliwa kama hafanyi kazi yake kuna ruhusa ya kumtoa kama wakati wake kufika. Tukasema pia Bunge litakuwa na nyumba mbili, National Assembly ya Bunge la hao 210 mtakaowachagua, pamoja na wale wataoteuliwa, halafu tutakuwa na National Council, Upper House, Bunge la wale wakilishi. Hiyo ni tofauti kubwa. Halafu tukasema kwamba kuna nafasi la wale wanaotaka kupigania viti hivi bila ya kuwa wanachama wa chama fulani, independent candidates, wanaweza kupata nafasi, sasa watasimamia. Mtu anaweza kusema anataka kura mwenyewe, chama gani hiyo wasema mimi sina chama. Haja yangu ni kura tu, mimi mwenyewe ninajitegemea, hiyo sasa inaruhusiwa.

Halafu tukasema Bunge hilo ambalo tumelichagua sasa limekuwa na nguvu sasa. Kwa sababu tumetoa nguvu ya ofisi ya Rais ambao wananchi walilalamika kwamba ofisi ya Rais ina nguvu nyingi, sasa tumezitoa nguvu zile na sehemu moja ambao tumezipeleka ni kwa Wabunge. Wabunge watakuwa na jukumu kubwa sana sasa. Watakuwa wale ndio wanateua na

kufuta hawa wafanya kazi viongozi wa uma, sio ofisi wa Rais tena. Watakuwa wao kazi yao sasa itakuwa ni full time, kila siku, sio ya siku mbili kwa wiki. Wanatatikikana Wabunge pia wawe ni wa form four walio pita, na baada ya kutoa zile nguvu kupeleka kwa Bunge pia tumeunda ile ofisi ya Waziri Mkuu ambaye atachaguliwa kutoka kile chama chenye ina Wabunge wengi. Huyu Waziri Mkuu atakuwa yeye ni Mbunge pia, atakuwa na manaibu wawe wawili. Halafu tumeandika kazi wa Rais ni zipi, tumeandika kazi za Makamu wa Rais. Waziri Mkuu ni zipi. Halafu tukasema kwamba ma-Waziri hawatatoka katika Wa-Bunge. Wabunge watakuwa mbali na mtu ambaye anataka kuwa waziri, atakuwa ni mtu mbali ambaye ameelimika katika taaluma ya ile wizara ile. Kama ni Waziri wa Ardhi, basi huyu mtu amesomea mambo ya ardhi.

Vyama vya kisiasa: tukasema vyama vya kisiasa hatukuviandikia number yake, kama vile vitatu au viwili viwili au arubaini, tumesema tumetoa masharti magumu ambavyo vyama vingi vitapotea tu hivyo hivyo. Kwa sababu tumetoa uhuru wa kufanya unavyotaka, tukaona ni vigumu tena kufinya kusema muwe lazima muwe kwa vyama vitatu au nne. Lakini vyama vile ambavyo vitakuwa vimepita ule vina uwakilishi Bungeni, tumesema vitapatiwa pesa za Serikali.

Halafu vyama tumeviandikia kazi zao. Vyama za kisiasa kazi zao zime andikwa, moja kazi yao kubwa ni kufanya civic education, kuwafundisha wananchi kuhusu governance, utawala. Sio kungojea mwaka wa kura ndio vifufuke, tumesema vifanye kazi hio. Tumesema vyama vizipo fanya kazi hiyo vina kuwa de-registered. Kazi yao ni kufundisha wananchi, halafu kazi yao nyingine kubwa tumewaandikia lazima vihusika katika maendeleo. Sio kupiga kelele tu za compaign. Wabunge hawatakuwa na uwezo wakuongeza mishahara yao. Tumechagua Tume ya kuangalia mishahara wa wafanya kazi wa uma kama hao. Kwa hivyo sio kazi wa Wabunge tena.

Halafu viongozi wote wa uma watakuwa na sheria za kufanya kazi yao, leadership codes. Kama mtu hazifuati hizo, basi atakuwa yeye anaruhusa ya kuondolewa. Moja yao hiyo ni kwamba wale wanataka kupigania viti kama hivyo ni lazima waeleze mali zao wamezipata wapi. Halafu tukasema ni Rais atachaguliwa na wingi wa asilimia hamsini, za kura zote na awe amepata asilimia 20 katika mikoa isio pungua nusu ya ile mikoa ya Kenya. Kama mikoa ni minne basi lazima apate asililmia 20 katika mikoa mitano. Wakiwa hawatapata wale wagombeaji wa uRais, tutachukua yule number 1 na number 2, watafanya round ya pili. Atakayeshinda huyo ndio atakuwa ni Rais.

Pia tumesema Rais anaweza kushtakiwa akiwa kazini, akifanya makosa na ikipatikana, kwamba ni kweli yuko na makosa anaweza kutimuliwa. Tukasema pia tumeondoa nguvu za Serikali kutoka Serikali ya Nairobi tumeleta kwa Serikali za mitaani. Tumesema kwamba tutakuwa na Serikali ya Kijiji, tutakuwa na Serikali ya Location, tutakuwa na Serikali ya Wilaya, tutakuwa na Serikali ya Majimbo. Halafu tumekuwa kwa sababu hio tumeondoa Provincial Administration. Tumeondoa machifu, manaibu, D.O. D.C. P.C. wote watarudishwa kwa ofisi ya Rais wakafanye kazi huko.

Halafu upande wa Mahakama tumesema kwamba wanachi wanalalamika kuhusu rufaa, tumeunda korti mpya inaitwa Supreme Court, iko juu ya Court of Appeal. Hiyo ndio Court Kuu kabisa katika Kenya sasa. Halafu ma jaji

tumewawekea, tumewapunguzia umri wao wa kufanya kazi. Tumesema badala ya miaka 74, wengi huwa ni Wazee sana, tumewawekea miaka 65. Ofisi ya Kadhi, Mahakama ya Kadhi tumeiunda mpya, Kadhi mwenyewe sasa atachaguliwa na Waislamu, pamoja na Judicial Services Commssion, halafu ma Kadhi tumewaongeza wamekuwa ni 30 badala ya 6, Kenya nzima. Tumeweka Provincial Kadhi, District Kadhi na Kadhi wa chini zaidi, na tukapanua kazi za ofisi ya Kadhi. Halafu tukaunda viombo vingi, lakini kimoja cha umuhimu ni kwamba tumeunda chombo ambacho wananchi watakuwa wanaweza kwenda kulalamika, kushitaki viongozi, bila ya kwenda polisi. Inaitwa Complains Office, ama Ombudsman, defender. Kama umehudhuliwa na askari, kama umehudhuliwa na nani, unaweza kwenda kushtaki na yule mtu akachukuliwa hatua bila ya kwenda polisi.

Halafu kufuatana kwamba tumeondoa Provicial Administration, hata wata wale Adminstration Police pia hawako. Sasa watajiunga na kikosi cha polisi, na ambacho tumekifanyia marekebisho tutakiandikia kazi zake kuifanya, tumewasema kwamba ni walinzi wawananchi. Kuna haki ambazo ni lazima wadumishe, kuna mambo ambayo ni wafanye, kuna mambo mengine hatutaki wafanye. Na tukasema tutawatrain vizuri hawa Polisi, wawe wanajua jinzi ya kushika watu vizuri, wawe wanajua kulinda usalama, wawe wanajua uhusiano baina wananchi na askari. Sio kwamba mkiona polisi mnajua kuna problem imetokea. Sihivyo sasa, wakitokea polisi hapa na gari yao wanazunguka badala ya kufikiria kwamba uko kwenye usalama lazima utuliza kumetokea nini. Sasa tunataka kuubadilisha na kuwapatia sura mpya Jeshi la polisi.

Halafu tumeunda pia haya majeshi mengine yako kwenye Katiba sasa, Jeshi la Angani, Jeshi la Arthini, Jeshi la Majini, yote yalikuwa yako kwenye Ministry ya Defence, sasa tumeiweka kwenye Katiba, na wakuwao tutaandika vile ambavyo watateuliwa. Uteuzi wa wakubwa, mambo yote viombo vyote hivi sasa ni Wabunge ndiyo wata aamua.

Upande wa ardhi, tumeunda Tume ya Ardhi ambayo itakuwa kazi yake ni kuangalia habari za mashamba Kenya nzima, hii Tume itakuwa na branches kila mahali, na hii Tume itachukua nafasi ya ile Land Commssioner, kwa sababu watu wame lalamika kuna corruption nyingi, mashamba yanatolewa kiholela, sasa tumewapatia Land Commssion.

Upande wa ardhi pia tukasema kwamba, ardhi iskuwa ni either ni za government, Serikali au itakuwa ni ya mtu binanfsi, private, au itakuwa ni ya wananchi. Community land: Community land ni ile Trust Land. Sasa imetoka kwa County Council, sasa itakuwa ni ya wenyeji wenyewe ndio wamepewa ardhi ile wao wana mamlaka ya kuifanya vile wanavyotaka. Halafu upande wa mazingira, tumesema kwamba Kenya ina shida wa mazingira, na tumesema sasa ni jukumu wa wananchi wote kuhakikisha kwamba wananchi iko katika mazingira sawa sawa. Halafu tumesema kwamba mali asili ya taifa hili ni lazima igawanywe vizuri inavyo wezekana sio kwamba iende kwa watu fulani au area fulani pekeyao. Sasa hizo ndizo tofauti kubwa ambazo tumezitoa katika hii Katiba mpya, ambazo katika ile Katiba ya zamani hazipo, na mlilalamika kwamba mantaka haya mambo yaangaliwe.

Tukienda kwa Katiba yenyewe, sura baada ya sura, utakuta kwamba Katiba hi sasa iko na utangulizi. Kumbuka hapa

watu walisema kwamba wanataka utangulizi katika Katiba, imeandikwa utangulizi mtauangalia, kama unatosha au hautoshi. Pia tukasema kwamba taifa la Kenya sasa tumelitangaza katika Katiba tumeliandikia vigingi vyake tumeviandika, ukivifuata vigingi hivyo utakuwa umezunguka Kenya nzima. Halafu muhimu kabisas ni ile sovreignity, ule uhuru wa watu. Mamlaka ya wananchi wa Kenya tumeyaweka mbele kabisa katika sura ya kwanza ya Katiba yetu, kwamba wananchi watazingatia maswala ya kisheria kwamba Katiba ndiyo sheria kuu inayo angalia mambo yote hapa Kenya, ya kwamba wananchi wote wako sawa mbele ya sheria. Nani anaweza kudumisha Katiba: tumesema kwamba ikiwa mwananchi anakuta kwmaba kuna mtu anavunja Katiba au haki zake za kiKatiba hazifuatwi, huyu anaweza kwenda kortini mara moja kudai haki yake ya kikatiba.

Halafu upande wa lugha tumesema sasa lugha ya taifa ni Kiswahili, ingawaje tumeendelea kusema kwamba lugha rasmi za Kenya basi ni Kiswahi na Kiingereza, lakini lugha ya taifa sasa rasmi officially ni Kiswahili. Upande wa sikuku za kitaifa, tumewacha sikukuu tatu, Madaraka day, Jamhuri day na siku ambayo Katiba hii itaitishwa tutataka hata tunapendekeza iwe ni sikukuu, hizo nyigine zote tumeziondoa.

Halafu pia tumeandika duties za citizens, kazi majukumu ya wananchi ni nini? Tumesema wananachi lazima wawe wanafuata sheria sio watengeneza sherial leo, halafu waivunje halafu waanze kulaumu Serikali. Sasa ni jukumu la wananchi kufuata sheria wao wenyewe. Halafu ni lazima wajue mambo yanayo tendeka baina yao. Utawala vinavyo endeshwa hasa ni kazi yao sasa kuangalia mambo yanaenda vipi. Tena ni lazima wahusika katika mabo haya sio kungoja kufikiria kwamba kuna watu fulani ndio wana wahusu, ni lazima wahusike. Ni lazima wananchi wawe wanafanya kazi. Ni lazima wawe productive, yaani wanatumia wakati wao mwingi kufanya vitu ambavyo vina faida kwao. Upande wa urahia, tumetoa sheria za kwamba ni namna gani mtu anaweza kupata urahia, nyingi nikama zile za sasa lakini tumeongeza tu wale ambao wana watoto au wameolewa na wageni, wale wanaweza kuwa ni rahia watoto wanaozalima ni wa Kenya, na raia, hata kama amezaliwa na mzazi moja, huyu akitaka uraia atapata.

Tuna ruhusu mtu akitaka kuwa raia wa nchi mbili, Kenya na Uganda, Kenya na Tanzania. Sasa nafasi iko lakini tunaweka vikwazo kama anaonekana atakiuka hiyo basi tutamtoa katika urahia wa Kenya. Upande wa uraia tumesema katika section 16, tumesema kila mtu anahaki ya kupata kitambulisho, birth scertificate na passport., kama anaitaka hiyo sio shida, lazima apatiwe.

Upande wa haki za kimsingi, ufisadi ni nyingi sana, kwanza ni lazima serikal ihakikishe kwamba haki hizi zinapatikana na itengeneze sheria, na tukasema haki hizi zote zinalindwa na sheria na utengamano wa wananchi, mila na desturi zao ni lazima wazifuate, na tumesema hasa tusiwe na ubaguzi wa aina yoyote. Ubaguzi wa rangi, ubaguzi wa kabila, ubazi wa dini, ubaguzi wa nini, kila kitu lazima sasa kiwe sawa. Akina mama nafikiri tulikuwa na shida hapo, akina mama mambo ya kurithi yale mambo ya usawa, tumewapatia haki zao, akina mama wanaweza kufanya vile wanavyotaka. Kulingana na mila sheria na dini.

Wazee: tumewapatia haki zao. Wazee hawana haja ya kubaguliwa kwa sababu ana mvi, kama Chairman wangu pale. Wanahaki ya kuhusika katika kazi zote za kujenga taifa hili kama kuna vyeo wanastahili kupata, ni lazima wapate msisemae hawa wazee wamemaliza umri wao, waende nyumbani wakalale, sasa tumesema kwamba *old is gold*. Kwa vile ambavyo wamepita umri wa miaka 60, au 55, wale wamebahatika sana. Sasa ni lazima tuwalee vizuri, badala kuwalaani kwamba hawafi hawa wakiondoka tukapata nafasi. Sasa tunasema kwamba ni lazima tuwaheshimu zaidi. Mtu kufika miaka sabini si kitu rahisi.

Watoto: hakizao zimeandikwa pale lakini haki moja umuhimu ilijitokeza ni kwamba elimu sasa ni bure kutoka nursery mpaka standard 8, na tumeeleza kwa nini itakuwa je ili ahakikishe kwamba ni bure; bure ile ya kweli, sio, ile ukifika kuna PTA kuna nini na nini. Halafu tukasema haki za wale wasiojiweza, wenye vilema, tumeeleza hapa, kwamba hao wana haki zao kama binadamu, si makosa yao kuwa namna ile. Haki za elimu lazima wapatiwe, lazima vifaa vyao vipatikane kwa bei rahisi, lazima kwamba usafiri yao uwe unaangaliwa, wakikwenda mahali isiwe ni shida, lugha yao lazima ikubalike, na wapatiwe. Kwa mfano tumekuja nalo ile Katiba ambao imeandikwa kwa lugha ya vipofu, tumempatia ndugu yetu hapa, na kisha kwamba wananchi wa Kenya wanawakuta hawa ni binadamu kama wao.

Usalama wa urahia tumesema ni jikumu la serikali, na kwamba ni lazima ihakikishe kwamba raia wamekaa vizuri wamelindwa inavyo wezekana. Religion dini na mahadi yake tumesema ni lazima wananchi wawe wanana uhuru wa kuabudu, bora wasiwe wanafanya vitendo ambavyo tumeandika, ambavyo zitakuwa vinadhuru ule uhuru ule, au vinahitilafu kwa wengine. Kwa hio tumeandika hapa maswala ambayo Waislamu kwa mfano walikuwa wanasema hawataki kutumia korani kuwekwa kwenye mahakama, tumeondoa hio, wakasema hawataki kuinamia jaji, tumeondoa hio, au kuwapa ambavyo hutaki, pia tumeondoa. Utaapa na vile unavyo fikiria ni sawa na mungu wako.

Freedom of expression tunaweka sawa, unaweza kujieleza vile unataka bora usitumie lugha chafu. Habari za kitaifa, sasa una haki wewe kutaka habari ambao zimewekwa za kitaifa zimewekwa na Serikali, wewe unahaki ya kwenda kutaka kujua kumetokea nini, sasa usiwe kwamba unafanyiwa fedha.

Freedom of association, tumeweka ni sawa mikutano imeruhusiwa. Sio lazima upate permit au nini, ni notice tu inatakikaana tunaandika kwenye section 49.

Vyama za kisiasa, haki za kisiasa tumeandika pale, tukasema kwamba anaweza kufanya compaign bila ya vita, na katika upande wa siasa tumesema kura zote zitakuwa ni za siri. Hakuna kura ya mlolongo wala ya kuinua mikono wala ya kupiga kelele kura ni za siri..

Upande wa wafanya kazi, tumesema wanahaki ya kupata mishahara vizuri. Tena wanahaki ya kufanya kazi katika

mazingara yanayofaa yakibinadamu, wanahaki ya kujiunga na vyama vya wafanya kazi, na wana haki ya kugoma ikiwa mambo yao hayafanyiki vizuri.

Halafu tumekuja kwa upande wale washukiwa, mtu ambae ameshikwa kwa sababu anashikiwa kwamba amefanya makosa fulani, tumesema kwamba hakuna torture, kule kuteswa ili useme maneno ambao ni ya uongo lakini ukubali; tumeondoa hiyo. Tumesema kuamba mtu mshukiwa hawezi kuwekwa kwenye cell moja na mtu ambaye tayari amesha hukumiwa. Tumesema mshukiwa akishikwa hasifike mahakamani kunapo masaa 48, ni lazima afikishe. Ikizidi hapo, basi kuna shida tumeandika tutachukua hatua gani. Halafu mtu yoyote ambaye amefikishwa mahakamani ni lazima ahukumiwe vizuri, apatiwe muda wa kutosha wa kujiandaa kuja kujitetetea. Sio kama leo umepelekwa halafu kesho tayari, na kama hutaki tayari, ndani rumande, tumesema apatiwe muda wa kutosha. Tumesema lazima kesi zifanyike haraka inavyo wezekana, sio kila siku kesi yatiwa tarehe. Tumesema ni lazima aweko pale kesi inapoamuliwa. Bila yeye hapaamuliwi kesi. Halafu tukasema kwamba mtu kama huyu pia ikiwa hana uwezo lazima apatiwe wakili wa Serikali, hasa ikiwa ni maswala ambayo kuhusu maswala ya kibinadamu yamekosewa, basi na hana huwezo lazima apatiwe.

Halafu tukasema wale ambao wamefungwa, wamepatikana na hatia wakahukumiwa vilivyo wakafungwa, wapatiwe haki zao. Kwanza wasishikwe kama ambao sio binadamu. Tumesema kwamba wasi dharauliwe, wasibaguliwe, wasitukanwe, wasifanyiwe dharau, kwamba hawatapata chakula kizuri, wapate nguo wakiwa jela, wapate malazi chakula afya na choo, vyoo vizuri. Sasa ni lazima wapatiwe. Pia madawa ni lazima wapatiwe au ni kama ni kama wana uwezo wenyewe wakuita dakatari wao ni sawa. Kama ni wafuasi ya dini fulani na imefika siku ya kuenda maombi ni lazima wapatiwe. Kama ni wa-Islamu wanaswali swala tano, tumeandika pale lazima waruhusiwe. Na tukasema kwamba wafungwa wa akina mama na wafungwa akina baba ni lazima wewe separated. Kila mtu awe na mahali pake.

Halafu tukaja upande wa uchaguzi, tumesema kwamba uchaguzi wote lazima uwe wa haki, lazima uchaguzi uwe wa siri, ni lazima uchaguzi ufanywe na Electorol Commssion. Hata uchaguzi wa vyama vya kisiasa. Kama wanateuana, nani atagombea, nani atakuwa secretary, pia utasimamiwa na Electoral Commission kwa sababu wanaoneana sana kule. Tumeunda Electoral Commission, tukasema kwamba Electoral Commission sasa itakuwa na wanachama wasio zidi 10, na kila mukowa utakuwa na mtu wake pale, tukaeleza, vyama vitaandikisha namna gani, Electorol Commssion itaandikisha vyama si hapa. saa hizi ni Registrar of Societies. Tumekuta kuna shida pale, kundi hili likienda linapatiwa certificate, kundi nyingine likienda linapata certificate, mtokwenda angalia wenyewe. Sasa tumesema ni Electoral Commission ndio itafanya kazi hio. Na kazi zake tumeziandika pale, moja ya umuhimu kabisa ni kwamba atafanya mambo ya civic education kuwaeleza wananchi mambo ya kura. Halafu tumesema pale tumeandikisha katika section 88, tumeandikisha orodha ya kazi, ni nyinyi sana kazi za vyama vya kisiasa.

Halafu tukasema kwamba upande wa Bunge ni kama nilivyo waeleza tumeandika sasa kazi za Wabunge katika secion 102, tumeandika kazi zao ni nini, ni nyingi sana karibu kazi kumi hapo tumeandika, wasipo zifanya mnahaki ya kuwatoa. Halafu

Wabunge ndiyo watakuwa wanafanya uteuzi, au kupitisha uteuzi wa viongozi. Kama ni mkubwa wa kilindini, kama ni mkubwa wa wapi, kama ni mkubwa wa Judicial Service Commssion, kama ni mkubwa wa nani, Teachers Service Commission, hawa wote, sasa hawa Bunge ndiyo litaamua ni nani atachaguliwa.

Halafu tukasema kwamba kulikuwa na shida ya kupitisha sheria, tukasema kwamba Wabunge likipitisha, sheria tunatoa wiki moja au mbili zaidi ikizidi ni lazima Rais awe ametia sign, hiyo ni sheria. Na tukasema watakuwa wana-serve miaka mitano mitano, na tumesema kwamba Wabunge ni mara mbili, lile Bunge la Kawaida ndiyo ambao watakuwa wanaserve miaka mitanao hawa Wabunge wetu 210, na tumesema wale wanakuhusiwa kupiganiwa watakuwa na miaka 21, paka miaka 70. Bunge lile la juu,. Lile la Upwer House litakuwa na Wabunge 100, wale watakuwa kila mtu lazima awe na miaka 35. 170-watatoka kila Wilaya, moja moja katika Wilaya itapiga kura kuchugua Mbunge wa wilaya, halafu wanne watatoka kila Mikoa, watakuwa akinamama. Kina mama 30, wanne wanne, kwa mikoa 7, wawili kwa mikowa Nairobi, hawo ni 30, pia nao mtawachagua nyinyi wenyewe.

Upande wa ----sababu ya kutengeneza majumba mawili ya Bunge ni kwamba, tulisema kwamba tunataka ile checks and balances. Bunge moja lisifanye mambo ambayo hayafai halafu hakuna mtu wa kuangalia. Kwa hivyo wale wakipitisha lazima wapelekwa wenzao nao wapitishe. Na Bunge litakuwa na ratiba yake maalum, sio mtu mmoja au wawili waje waseme leo navunja kesho mtaanza hivi, au wakiona kuna mambo hot ambao wanadiscusiwa Bunge linavunjwa, sasa tumepatia Parliamentary Service Commission. Watapanga tarehe ngapi mpaka tarehe ngapi, Bunge litakaa tarehe ngapi, itaenda lini tarehe ngapi, namna hio. Wao wenyewe wataangalia mambo yao.

Halafu tukawaeleza upande wa utawala: Rais tumesema kazi zao tumeziandika pale, huyo ni mkubwa wa kitaifa, kazi zake tuemeziandika pale. Halafu tukaeleza kwamba yeye atakaa miaka mitano, akizidi kabisa ni miaka kumi. Umri wake ni miaka 35, mpaka 70, na kama amefanya makosa anashitakiwa, akipatikana anaondolewa. Ofisi ya Makamu wa Rais tumeandika kazi zake pale ni nini. Ni lazima atakuwa ni running mate huyu, wakati ule wanatangaza uchaguzi, pia ameshatangaza makamu wa Rais ambaye atakuwa anafuatilia huyu mgombea. Halafu tumesema kuna Waziri Mkuu na Manaibu wa MaWaziri wawili, wote watachaguliwa na Bunge, na Mawaziri pia watachaguliwa na Bunge, na tumesema, maWaziri sio wa Bunge. Mahakama vile vile tulivyo eleza kuna ratiba vizuri kazi zao ni nini, tumeandika vizuri pale, kuna korti vile za kawaida, Magistrate Courts na Kadhi's Court, halafu tuna High Court, tuna Supreme Court, tuna Court of Appeal, halafu tuna Traditional or Local Tribunals. Wazee walisema wanataka kesinyingine, hazina haja kwenda Kwale, kuna case ndogo ndogo, hapa nyumbani tunaweza tukaziamua tumewapatia nafasi hiyo. Tutaandika jinzi ambavyo zitaundwa lakini ziko Traditional or Local Courts ziko. Hata ma-Judges pia tumesema watachaguliwa na Bunge.

Serikali za kitaifa: tumesema kwamba sababu moja watu walilalamika ni kwamba Serikali ambayo iko Nairobi imeshindwa kupatia wananchi huduma zinazofaa, iko mbali sana. Sasa tumegawanya mamlaka Serikali ile ya Nairobi itakuwako, Serikali ya Majimbo itakuwako, Serikali ya Wilaya, Serikali ya Location na Serikali ya Kijiji. Serikali ya Kijiji itakuwa na

wanachama 6 mpaka 10, wasi zidi 10, wasipungue 6. Wananchi wenyewe wataamua, wamepewa uhuru wa kuamua kama watawachagua kwa uchaguzi wa siri, au wata wateua. Hilo ni jukumu lenu. Kutoka pale wawili kati ya wale wataunda Serikali ya Location halafu Location itachagua directly ni nani atakuwa Location Adminstrator, sawa sawa na ile Councillor wa sasa au Chief. Ana changanya kazi zote mbili huyo za Chief, na za Councillor zitakuwa ni za mtu mmoja.

Halafu District government itachaguliwa na wananchi wenyewe. Kutakuwa na wanachama wasio pungua 20, wasio zidi 30, hiyo ni Serikali wa Wilaya, District Government. Wale wanaotaka kugombania viti hivyo wata jitangaza wenyewe katika District nzima. Tutawaopigia kura sisi wenyewe. Yule anataka mkubwa wao, District Govenor, ni kama Chairman wa County Council, huyo naye atakuwa na debe lake mabli. Watakuja wale wanaotaka, watagombania, tutawachagua wenyewe. Halafu Serikali ya Majimbo wale wawili, kila jimbo itachagua watu wawili lipeleke katika Serikali ya Jimbo ambapo hapo watachaguana ni nani mkubwa wa Jimbo hilo, official govenor. Na tukaandika kazi zao ni vipi. Kila Serikali imeandikiwa kazi yake pale, lakini kazi nyingi zitafanywa na District na jimbo. Kazi zote sasa, sio upande wa Serikali tena. Kazi zote zitafanywa na Serikali ya Jimbo na Serikali ya Wilaya. Tumeziandika katika schedule 5, ukiangalia huko nyuma utakuta tumeandika kazi zote ambazo wanatakikana kufanya. Hata kuajiri askari, kuajiri wafanya kazi, kila kitu ni chao hao. Kwa hio msianze kuwalaumu mamlaka yametolewa kule mlikuwa mnalalamika yameletwa chini Ikiwa tumechagua Serikali hizi tumechagu, zikikosea pia mnahaki ya kuzitoa nyinyi wenyewe. Tukasema kwamba mji kama Nairobi au Mombasa itakuwa Serikali yake ni za--- zote ambazo ni miji Mombasa au municipalities zitakuwa ni kama Districts, zitachaguliwa ni kama Districts, ile vile ni sawa sawa na Serikali ya District. Town na urban centres zitakuwea na Serikali kama za Location. Na hizi Serikali zote tumeandika zile functions zao, tumeandika ambavyo wataweza ku-share resources, ku gawanya resourcess tumeandika, wanahusiana vipi, wana haki ya ku-cooperate.

Halafu upande wa ardhi, kamanilivyo waeleza pale nimesema wananchi wote wanahaki ya kupata ardhi kama wanaitaka, Serikali ikiwezekana ipatie watu mikopo ili wanunue ardhi. Hilo pia tumeliandika. Halafu tukasema kwamba ni wananchi wenyewe ndio watamiliki ardhi yao, wao wenyewe. Kwa hivyo yale maswala ya zile kaya mlikuwa mnaliya sasa zimeletwa kwa wenyeji. Wenyewe ndio wataangalia saa ya zao, ile sehemu ambazo ni za maombi, sehemu ambazo ni za mila zote zitaangaliwa na wenyewe. Lakini la muhimu tumesema ni wageni hawata ruhusiwa kuwa na ardhi Kenya. Mtu ambaye sio rahia wa Kenya, sasa itakuwa ni marupu rupu kuwa na title deed ya land. Wale watapata lease peke yake wanakodisha tu kwa miaka --- kwa njia ambayo haifai, ardhi ya Serikali, lazima katika miaka miwili baada ya Katiba hii iwe hiyo imechunguzwa na imejulikana na kama ni kurudisha kwa wanachi irudishwe au kama ni lipa rizaa ilipwa, imeandikwa kwenye section

Halafu tukasema kwamba ikiwa kuna mikataba ambao ilifanywa zamani kuhusu ardhi katika Mikowa wa Pwani, Eastern, Rift Valley na Mikowa mengine mambo ya akina Mazrui hayo, mambo ya 10 miles Coastal strip iangaliwe yote, halafu yawezekana kurudishwa kwa wenyewe au kulipwa ridhaa, zifanyike namna hiyo.

Upande wa madini, ardhi, madini katika ardhi, tunaandka katika section 238, kwamba sasa, sio kwamba ikigundulika kwamba kuna madini, ardhi si yako, ardhi ni yako hata kama kuna madini, hiyo ni yako. Upande wa Environment, hapa tulikuwa na swala la wanyama wa pori kusumbua wananchi, sasa tumesema kwamba watalindwa na ikiwa kuna yale madhara ya kuuliwa, sasa tunasema adequate compensation, lazima walipwe ridhaa, na tumesema kwamba Serikali nilazima ihakikishe kwamba inalinda mazingira ya binadamu na ya wanyama halafu wananchi ya sehemu zile ndio hawo wata husika zaidi. Na tukaunda Tume ya Mazingira, National Environment Management Commission, tumeiunda hiyo, kushirikiana na wananchi wenyeji, ili wahakikishe kwamba maswala ya mazingira inaangaliwa vizuri. Upande wa fedha za umma, tumesema siruhusa mtu yoyote kutosha watu kodi bila kupitia kwa Bunge. Kodi zote sasa ni lazima zitatokea kwa Bunge, lazima Serikali ya jimbo kama inataka, lazima iandike kwa Bunge, Bunge lipitishe, Serikali ya Wilaya kama inataka kutosha kodi akina mama mahamri haya kwanza lazima iandike Bunge wajadili wakikubali ndiyo inapitishwa.

Upande wa makadirio ya fedha kila muaka tumesema kwamba, miezi miwili kabla siku makadirio ya fedha, budget, wananchi watakuwa wamejadili kwanza. Watahusishwa katika budget ya Serikali. Wajue tunataka pesa ngapi, tutafanya nini tupate pesa zile halafu ndiyo Waziri wa fedha sasa atakwenda Bunge, wananchi tayari wameshajua kutasemwa nini.

Halafu tukaweka Central Bank, sasa Benki Kuu ya Taifa sasa imewekwa katika Katiba. Zamani ilikuwa katika wizara. Sasa tumeiweka katika Katiba, tutachagua govenor wake, tumeeleza atachaguliwa na Bunge, na kazi kubwa tumeziandika, kazi za Central Bank, tumeandika moja wapo ni ya kutengeneza noti na shillingi vile, la muhimu ni kwamba isiwe na picha ya Rais alioko.

Public servcie, tuna ile Tume ya Public Service tumeiweka vizuri, tumeiunda vizuri tukaeleza maadili ambayo wafanya kazi wa uma ni lazima wayafuate, tukasema hata hawa polisi tumeandikia kazi zao katika section 264 tumeita Kenya Police Service, badala ya Kenya Police Post, tukaandika kazi zao pale karibu 7 tumeziandika, ni lazima wahakikishe usawa wa wananchi, lazima wa prevent crime, ukora ukora ule, lazima wawe ni watumishi, sio mabwana. Halafu tukaandika pia mkubwa wao atakuwa ni mtu ambaye amehitimu shahada ya degree, mkubwa wa polisi. Awe lazima amekuwa askari kwasaidi ya miaka kumi. Na atafanya kazi pale, hata yeye hata zidi miaka kumi.

Upande wa jela tumeziita Kenya Correctional Services badala ya Kenya Prisons, na pia yeye mambo yake kama hiyo tunaandika kazi zake, director atachaguliwa vipi, atafanya kazi miaka mingapi. Kama nilivyo eleza tumeunda ma-places sasa. Tumeunda Security Council, National Security Council, mkubwa wake ni Rais, na atakuwa pale na makamu wake, Prime Minister atakuwako, Waziri wa defence, wakuu wa Majeshi watakuweko wote. Kwa sababu ya kwamba huyo ndiye mwenye kiti atakuwa ni Rais, kwa hivyo bado yeye kumaliza kazi atakuwa ni Mkuu ya Majeshi haya ya Kenya nzima. Halafu tutakuwa na sheria ambazo wafanya kazi waskari wa umma lazima wazifuate, tumeziandika hapo chapter 16.

Halafu tumeunda tume nyingine mpia, na zile za zamani tumeziandika vizuri. Tumeunda Tume Moja kuibwa inaitwa

Commission ya Human Rights. Haki za ki binadamu, haki za kimsingi. Tumeieleza vizuri, ndani yake kuna sehemu ya Tume ya Akina Mama, mambo yua maswala lya akina mama, tumeweka pia ile Public Defender, ile ofisi ambao mwananchi wa kawaida anaweza kwenda kulalam, la kwamba kazi yake haikufanyika. Au anaweza kushtaki askri au kiongozi ambaye ana hakika amevunja sheria, au mwananchi ambaye hataki kufuata Katiba.

Pia tukaunda hiyo Salaries and Remuneration Commission, ya Mishahara. Halafu katie Tume ya Katiba ya kuangalia utekelezaji wa Katiba hii pia tumeiweka pale na wanachama watano.

Halafu mwisho tukaandika kubadilisha Katiba. Tumesema kwamba Parliament au Bunge bado itakuwa na kufanya urekebishaji wa Katiba isipokuwa maswala fulani ambayo yameandikwa pale ambao ni lazima iwe ni kura ya maoni, ndiyo yabadilike, sio kazi yao sasa kubadilisha bila kuwashauri wananchi. Tumeandika pale kama ni swala lina kuhusu huru ya wananchi, masilahi ya wananchi wa kawaida, swala hilo ni lazima lifanyiwe kura ya maoni. Mipaka ya Kenya, kura ya maoni, Serikali za Majimbo na za mitaani, kura ya maoni. Uraia wa Kenya, haki za kimsingi, kura ya maoni. Hizo vitu vyote hizo haibadiliki mpaka wananchi wenyewe wakubali. Kwa hivyo tutakoma hapo, nafasi hii ni yenu. Ikiwa kuna jambo ambalo mulisema halipo, mseme mnafikiri halipo, mseme, au limeletwa vile ambavyo hamukutaka msema, au mnataka litolewe mseme. Uhuru ni weni, maana uhuru wa kusema vile mnavyotaka, sisi kazi yetu ni kusikiliza na kutekeleza. Haya asanteni.

Kwa hivyo nitawapatia nafasi, mtu yeyote anayetaka kuongea, ainue mkono, nitawapatia nafasi, uwa ninachukua watu kumi kumi. Sio ile pombe, lakini ni hesabu ambayo inatufaa sana. Kumi kumi, wale kumi wa kwanza wanaotaka kuchangia. Wa kwanza ni huyu, wa pili, tunataka tuwajue kwanza. Wapili, kila mtu nitampa number yake, nikisema number 2, unajua ni wewe. Nikisema number moja, unjua ni wewe, msichanganye. Haya wa kwanza wa pili wa tatu, mzee wangu watatu, wanne ni nani? Aha, wanne yule pale, we uko number nne nikisema number nne ni wewe, wa tano, aha, wa tano, msiogope. Wasita ni Mzee wangu hapo nikisema number sita mzee utainuka wewe, eh, nikisema number sita ni wewe. Kule kwingine tulikuwa tukisema hivyo mikono mia moja imeinuliwa mpaka hujui utawachagua vipi hao kumi. Leo mbona---haya tuanze na hao sita, number one.

**Rev. Peter John Katana**: Kwa majina mimi ni Rev. Peter John Katana. Yangu ni shukrani kwa ajili ya Tume hii, kwani yote ambayo tumeelezewa ama kwa hakika yale maoni yetu ambayo tulikuwa tumeyatoa na kwa upande wangu karibu yote ambayo tulikuwa tumeiandika na tuka peleka tukaongea karibu mengi yameweza kutajwa. Kwangu mimi binafsi ninawashukuru sana Tume hii. Jambo ambalo ningetaka niongee ni kwamba ninasitikika kidogo kwa sababu tumekua tukisikia tu kwamba labda ni Serikali ama ni nani anasema kwamba labda Tume hii imeleta Katiba ambavyo kulingana na haya ni wananchi wenyewe ndio ambao tumeweza tukaleta wala sio Tume. Tume imekusanya yale maoni na imedhihirika kwa sababu baada ya kutusomea, ni yale yale ambayo tuliweza tukayaandika na tuka yapeleka. Kwahivyo langu si kwa kuwa ati nilikuwa nina jambo lingine la kuongeza lakini ili kuwa ni shukurani kwa ajili ya kazi hii ambay imefanywa. Ama

kwa kweli tumefurahia na vile walivyo tuahidia bada ya, mkishaenda mimi ni mmoja wa providers, mukishaenda kufundisha na wananchi wakielewa na kutoa maoni, kabla hakuja kuwa na lile Kongamano la Kitaifa, tutarudi tena na ukweli ahadi imeweza kutimia. Kwa hivyo shukurani yangu ni kwa ajili ya tume Tume, Mungu awabaariki sana.

**Mzungu Dzuya**: Kwa jina langu kamili ninaitwa Mzungu Dzuya kutoka Ndavaya. Mimi nili kuwa na maswali mawili. Swali langu la kwanza ni kwamba wati tulipo kutana hapa mwezi wa nne tarehe 30, tulitoa maoni kuhusu kwamba kiwer kita rotate katika hizi provinces zingine. Na hapa katika kuona katika ukurasa wa kwanza mpaka tukafikia, kiti cha Rais sijui kwamba kitakuwa na uwezo gani, ama kuna posts zingine hazita pata—hawata enjoy hiyo Urais. Swali langu la pili ni kwamba kiwango cha elimu cha Macouncillors hapa kwenye Draft sikusikia ikitajwa. Sijui Tume nayo hapo iliweka kiwango hiki kiwe vipi? Nimesikia ya Wabunge kwamba awe form four with a pass. Asante.

**Com. Swazuri:** Number tatu, number tatu----

**Itsika Ngala**: Mimi ni Mr. Itika Ngala. Nimetoa shukurani kwa mambo tuliyo yazungumza hapa soteni, na yametoka sawa bila kuwa makosa. Lakini kuna kitu kimoja, ambacho siku kipata. Watu wengine walifanya kazi Serikali, na walipofanya kazi na Serikali, wanapata ile pension. Na kwa hivyo hio pension sikusikiaik ikitajiwa kwamba watakuwa wanaendelea kupata au hawata endelea kupata. Asante.

**Com. Swazuri:** Wa nne----

**Michael M. Mwangada**: Mimi kwa majina ni Michael Mwangadu kutoka Taru. Mimi lile Kongamano letu la kwanza la kutoa maoni ambao ilifanyika Samburu, tuliongea juu ya elimu ya bure kutoka nursery mpaka darasa la nane. Tulikuwa tena tumependekeza kuwa kuwe na misaada ama mikomo ya elimu ya juu kuanzia form four mpaka ile level yoyote ya education mtu atakuwa ameenda. Kwa hivyo ningependa hiyo kitu kama pengine haiko hapo, amoni yangu kiongezwe.

Halafu upande wa afya, tuliongea kuwa kuwe na afya bure, na ikiwezekana haya mambo ya ma-private hospitals itupiliwe mbali kwa sababu hawa ma-daktari ambao wanao hudumu katika hospitali za Serikali, ndiyo wale wale wanaprivate hospitals tena ana his chemist. Sasa anakuandikia karatasi anakuambia enda chemist fulani, kumbe hiyo chemist ni yake. Pesa zinaingia kwake hivyo. Kwa hivyo ni maombi yangu kwamba ifutiliwe mbali haya mambo ya private hospitals na chemists ambazo zinaendeshwa na madaktari.

Halafu upande wa biashara, mimi ningependekeza Serikali ifutulie mbali uagizaji wa bidhaa duni. Na pia uagizaji wa bidhaa zinazopatikana hapa kwetu kwa mfano kama sukari tunapata hata jice ambazo tunaweza kutengeneza tu na maembe ama mananasi ambayo yanapatikana hapa kwetu yanaagizwa kutoka nje. Bidhaa kama zile zitupiliwe mbali. Halafu kwa upande mwingine, ni upande wa KBC. Sa hii ukifungua KBC itasikia tu mambo ya Kanu, wanchi wote wa Kenya si watu

wa chama kimoja. Kwa hivyo kama tutasikia mambo ya habari tusikie mambo ya vyama vyote. Kanu sijui Rainbow Alliance na kila kitu. Tujisikie mambo ya chama kimoja. Kwa hayo machache nimesema ahsanteni.

**Com. Swazuri:** Number tano---

**Libin Kesi:** Yangu ni mambo ya---ishazungumzwa tayari lakini ninona niongeze kidogo. Tuliyazungumza mambo wakati mlipo kuja, mambo ya pension. Mishahara inapoongezwa za watu wengine watu wa pension hawaongezwi. Hiyo si----mtu, hawawezi kuangaliwa. Hata akisha kufa amekufa basi. Atatupwa labda na watoto wanao soma huko nyuma hakuna chochote. Ama wengine wamechukuliwa na ukimwi, hakuna chochote ya kuangaliwa. La pili sikuelewa sawasawa vile ati Wabunge, Mawaziri hawatoka kwa Bunge, hapo ndio ningetaka ufafanuzi kidogo. Watatoka wapi? Asante.

**George M. Ngoloko**: Mimi kwa jina naitwa George Mwabaya Ngoloko, nina shukurani kubwa kwa kuwa tulikuja hapa tukaweka maoni yetu, kama hivi tulivyo. Na leo hii ni siku ya kuletewa yale majibu na kusumuliwa vizuri na ile tume ya Katiba, kwa hivyo nina furahi kabisa hakuna chochote ambacho kimekoseka katika upande wangu. Lakini mambo matatu ambayo sijui nimekuja nyuma maana nimeingie sasa hivi, sijayasikia, tulidai hapa kwamba Rais mtukufu Moi, wakati kama yeye hivyo angesimama si angechaguliwa tu. Basi akichaguliwa vile na ni wananchi, vile ambavyo amechaguliwa na yeye mwenyewe atasema hebu nichague Wabunge maalum, mimi hasa nilikata kusema kwamba Mbunge maalum hakuna nafasi ya kuchaguliwa na mtu binafsi. Achaguliwe na wananchi vile vile. Tuka rudi hapo tukasema, mimi hasa nilisema kwamba sikusikia hapo, ma chief nilizungumza kwamba kitoto kidogo kisome huko kinasomeshwa na baba yake, atapasi nafasi, na yeye hajui kwamba upande wa Location ni nini, maana siku zote yuko sikuli. Hajui mambo ya Location ni kwamba inaendeshwa vipi. Leo tunamkuta yeye ameandikwa chief kabla ya kuchaguliwa na wenyeji wenyewe. Hapo hiyo si sawa kabisa. Serikali yetu inayo kuja tunataka machief, manaibu machiefu wachaguliwe na wananchi wenyewe, wasichaguliwe na Serikali.

**Com. Swzuri:** Jambo la tatu----

**Ngoloko:** Tatu ni ndovu, ndovu ambao wanamaliza binadamu, na yule Waziri wa ndovu, ndovu akiuwawa halafu unatafutwa wewe mwananchi, ufungwe na upokonywe zile pembe za ndovu. Lakini ndovu akiuwa binadamu, na matunda ya binadamu, pale pale ni rahisi kwa --- hakuna malipo pale, hata lile neno ni makuruu kabisa kabisa. Hilo ni la tatu. Nne Majimbo, tulizingumza hapa sisi siku hiyo kwamba Serikali yetu tukufu inayo kuja iwe ya Majimbo. Sio kutakuwa mtu katikati ya mkubwa zaidi ikiwa ataketi katika hapo katikati ya, yeye ni mkubwa wa Majimbo, aweko, ikiwa ni hvyo basi. Lakini Majimbo yenyewe ajitawale vile vile, wenyewe kwa wenyewe. Nafikiri hapo nitakomea.

**Michel Matano:** Kwa majina ninaitwa Matano Mateke. Inatoka Ndavayo, katika Shirika la jamii, Kema Simio. Maswali yangi ni mawili yanayohusu kisheria. Kwanza, ufafanuzi wa sheria umruhusika katika Katika yetu, hushike katika

ngazi ya jamii au katika Serikali za mitaa. Lakini haikufafanuliwa rasmi kama vile ilivyo ruhusiwa katika kisheria ya ngazi za juu. Sasa hatujui huwa ni katika ngazi ya tarafa au ni katika Location, au itafikia hata vijijini hua watu wanaweza kuwa na ile ilikuwa ikiitwa baraza la Wazee kuhusiana na mambo ya kisheria. Katiba haikuwa na ufafanuzi rasmi aina hiyo.

Pili ni rasilmali zetu. Kuna maeneo kama yale yanao toa maji au chemichemi ambayo inahitaji ulinzi kamili. Sikusikia kikamilifu yamelindwa kivipi, maana kungeli sa hii, kuna uharibifu wa aina hiyo. Na kama ndivyo, kisheria sehemu kama zile zitalinda sehemu zile ki namnagani ili tuwe na maji ya kutosha kama vile inavyo elezwa katika Kenya nzima kuna shida ya maji, au rasilmali hii ya maji ina matatizo sana. Nazo tukilinganisha katika eneo letu na hinterlands.

Na mwisho kuna matatizo mengine yanayojitokeza katika rasilmali zetu hivi, katika Idara ya Forerst, watu wengi wana miti hii ya kienyeji, au wengine wanajipandia miti wenyewe mashambani. Sasa imekuwa ni vigumu sana kutumia ile rasilimali bila kupitia katika Serikali. Mtu ana mti wake shambani au amepanda miti yake shambani lakini ita mgharimu pesa mingi sana kufikia kupata kibali kuenda tumia ile rasilmali yake. Ni kwangazi gani ambao imepewa mtu wa jamii wa kawaida afikie huduma ile kwa Serikali mpaka hua anaweza kutumia ile rasilmali kwa njia inayofaa.

**Mwero Khaema:** Langu ilikuwa ni kuhusu elimu. Nimesema kwamba ni lazima----

**Com. Swazuri**: Sema jina—

**Mwero**: Ninaitwa Mwero Kaema. Hata nimesema kwamba kila mtoto ana haki ya kusoma primary free, hapo ni sawa. Ninataka kueleza vile kwamba yaani katika msururu huo huo wa elimu kwamba kila District iwe na national school, na pendekezo lingine ni kwamba kila province ni lazima iwe na university. Mandatory, kila province iwe na university, at least iwe ni lazima. Hapa Pwani, watu wa Pwani wote lazima wajitembeze mpaka Nairobi huko kupita ndipo asome elimu ya juu. Kwa wakati nyingi sana wengine wazazi hutishika kwamba watu wao huko hawatarudi salama kwa sababu ni mbali ama watishika pia ile expenses za kutembea, pai matemebezi kutoka sasa huko hua ni ghali sana. Shukrani.

**Emannuel Mwachuti**: Mimi langu nilikuwa nataka kwa sababu wakati tulikuwa hapa, jina mimi ninaitwa Emmanue Chiboya Mwachiti, na nickname iulongo wa kila mtu. Ninasema wakati tulivyo kuwa hapa tumejadili mambo ya mnazi, na nimeangalia hapa siku yasikia habari zake lakini ni pato kubwa lilileletwa sisi hapa. Sijui kama wale walikuwa hapa hawakuandika ama mlimesahau? Hilo ndiyo lilikuwa swali langu.

**Joseph Pili:** Kwa jina ninaitwa Joseph pili. Kwanza nataka nichukue nafasi hii, ni shukuru Tume ya Marekebisho ya Katiba kwa kuweza kufanya bidii kwa kila liwezalo kuweza ku transcribe maandishi yale ya print mpaka katika maandshi haya yetu. Kwanza Commissioner kwa niaba ya Tume pokea shukrani zangu nyingi na zetu nyingi sana wakati hii ambayo mumefanya. Kwa kweli ni vigumu ku transcribe kutoka kwa numbers za watu wanao ona mpaka wanambaa hizi zetu kwa kweli sio kazi

rahisi.

Nikija kwa upande wa kutoa maoni kuhusiana na marekebisho ya Katiba, ningependa niseme kwamba kuna mambo ningependa katika Katiba ijayo, yaweze kufanuliwa zaidi hasa kwa upande wetu sisi walemavu. Kwanza ni kuhusu ushuhuru, kwa sababu utakuta katika hospitali hizi zetu za serikali, na hata za private, utakuta ya kwamba tunafinywa sana. Hata katika magari ya abiria, maana utakuta ya kwamba ukiingia katika gari ya abiria makanga atasema ameiingia je ama ameona je mlango wa gari, na ilihali yeye haoni? So hapa ningependelea kama Kongamano la Kitaifa tume itaweza kufafanua zaidi kwa undani, na ikaweze kuanalyze, katika report hii, kabla Kongomano hii la kitaifa.

Halafu ushuru katika majumba uondolewe kwetu sisi walemavu. Halafu tena, mengine ni kwamba, haki jamii itutambue, yaani ninapo sema jamii let me say, kuanzia pale nyumbani, katika community. Kwa sababu, kama ni uzazi na kama ni jamii yoyote, pengine inatuchukulia watu duni, pia hiyo katika Katiba iwe ni sheria mtu kama huyo anapo tuchukulia kuwa watu duni pia yeye anahaki ya kushitakiwa na kuwekwa ndani. Kwa sababu itakuwa si haki na ita kuwa ni hatia na kinyume cha sheria kwa sababu sisi tutakuwa ni kama ambao' let me say, itakuwa ni ambao tunachukuliwa ni kama watu ambao yaani tunarudi katika lile itikadi ya kitambo ya kwamba kipofu atafanya nini, kiwete atafanya nini, kiziwi atafanya nini, bubu atafanya nini, etc, etc. Sasa mambo kama hayo ningependa Tume ijaribu kufafanua vile wameandika ijaribu kufafanua ili Katiba ijayo sasa iwe kuna uhuru ndani na nje ya mipaka yetu hata tukitembea hakuna wasi wasi. Asante.

**Com. Swazuri:** Haya asante sana. Nitaanza na Bwana Reverend, wewe ulikuwa unatoa shukrani tu. Lazima sisi wenyewe tunasema kwamba imekuwa ni kazi ngumu. Tumepigwa vita kila siku, tumetukanwa, tunaambiwa hatuelewani, kila aina ya neno sisi tumelisikia, lakini kwa sababu tuliapa kwamba tutaendelea na kazi hii mpaka mwisho, sisi tunaendelea, kwa sababu uzuri wa sheria yetu ni kwamba inasikiliza maoni ya wananchi. Sisi ni kama kapu tu ya kuokota na kupeleka. Kwa hivyo sisi tulisema hata watu wakitutukana vipi, watu wakituambia nini, lakini sisi tunafuata sheria; tunataka kutoa mfano kwamba ukifuata sheria, maneno yote yanawezekana. Na ninafikiri wale ambao wanasema kwamba haya ni maoni yetu, ni akili zetu si maoni ya wananchi, either hawajasoma ile Katiba wakaona au hawakuweko wakati wananchi wakitoa maoni wakazisikiliza. Hao ni wale ambao wamezoea kwamba tume ikichaguliwa hazitowi matokeo. Sasa sisi tumesema kwamba sisi tumekuwa tume ya kwanza kutoa matokeo kurudisha kwa wananchi, pengine imewaudhi watu wengine namna hiyo.

President awe ana-rotate kwa kila region, hiyo ni kweli, hatukuiandika. Tulizungumza sana, lakini mwisho tukasema wacha tusikilize wananchi watatuambia nini zaidi. Lakini tuliiwacha hivi, kwa hivyo tunaiangalia bado kabla Kongamano tutakuwa tumeiingiza. Halafu na qualifications za councillors, tulikuwa tumeziweka ni form four, lakini nafikiri hatukuiandika hiyo tumeambiwa mara nyingi. Bwana Ngala, pensions haziondolewi na Katiba. Pensions bado ziko, zitaendelea. Swala ambalo hatukuliangalia vizuri, lile la pensions kwamba iongezeke wakati mshahara wa mtu wa kawaida inaongezeka. Hilo ni swala ambalo tutaenda kuliangalaia.

Free education tukasema kwamba tunataka---- sisi tumesema kwamba baada ya standard 8 kule mbele, elimu gharama ya elimu irudishwe chini. Tumeandika hiyo. Serikali itafanya yoyote kuhakikisha gharama ya elimu ya kule juu made affordable. Either kwa kupatiwa bursary nyingi au kwa kupatiwa misaada zaidi. Hiyo tumeandika kwa upande wa education.

Halafu upande wa madakatari kwamba kama wanafanya kazi hospitalini, wasifanye kaze kwenye private clinics, hatukuandika katika sheria hizi lakini tumeandika katika heria za codes, intergrity code, katika shedule ya 5, utasomea pale kwamba tumesema public officer yoyote hawezi kupata mshahara miwili, ikiwa ile kazi anayo fanya kule nje ni sawa sawa na ile anaofanya kwa serikali. Hatukutaka kusema kwamba daktari asifanye kazi, engineer asifanye kazi nje, na tukawataja wote, aha, tulisema public officer pamoja na daktari ni public officer. Kama yeye anafanya kazi kwa serikali, huyo ni officer wa serikali. Tumeandika pale ukisome tumesema, haruhusiwi kufanya kazi ambayo itamletea mshahara iwe na yeye bado ana ajira nyinge za serikali. kwa hivyo hiyo automaticaly daktari sasa hawezi kufanya kazi kwa clinic ya nje. Itabidi aamue huku au kule.

Serikali isilete vitu, isiagize vitu kutoka nje. Kwanza nataka kusem,a kwamba kuna sehemu ambayo haiko kabisa katika katiba bado tunaiandika, ya kuhusu agriculture. Ukiangalia katika katiba yetu, haina mambo ya ukulima. Tulioweza kwa sababu hatukuweza kuimaliza, maanake hiyo ndiyo uti wa mgongo wa taifa hili. Lakini ilikuwa ni nyingi sana kwa hivyo sheria zake bado. Kuna watu ambao tumewacha wanaziandika tukifika tuzijadili. Kwa hivy swala hili la slukari, maziwa, mchele, vitu ambavyo vinapatikana hapa siku hizi hata tomatoe, mayai, zinapatikana hapa lakini zinaruhusiwa kuletwa kwa sababu ya hongo, hilo ni swala ambalo tunalijadili.

KBC should be fair to all, hata sasa hiyo sheria iko kwamba wawe wanatangaza kwa kutoa nafasi sawa za utangazaji kwa watu wote. Lakini kama uukisoma gazetti la leo hawa watu ambao wana TV, waliangalia mkutano wa jana wa Kalonzo Musyoka, alisema yeye alikuwa ndio waziri, lakini hawalalumu KBC, KBC wanafuata wanavyo amurishwa. Nafikiri katika gazetti limeandikwa hapo. KBC wanaambiwa msiseme kitu fulani, msiseme kitu fulani. Sio wao kwamba wao haja yao ni habari, lakin wanaamrishwa, kwa hivy ile sheria tumesema katika freedom of expression, tumeandika pale.

Mwananchi ana haki ya kupata habari zote kutoka vyombo vyote. Tumeandika katika rights za access to media. Sasa ule ni mtenda kazi tu wa pale. Lakini sheria iko ambayo inasema ni lazima wawe wanatoa habari za mambo yote yanayo tokea. Saa nyingine mimi ninli sikiliza mpira siku moja ambavy tear gas mimi naona kwa TV, kwamba kuna tear gas, wachezaji wamekosana wanapiganan, na tear gas imetolewa pale, lakini rafiki yangu Alim Manga bado yuasema kwamba tunangojea referee apige kitenga, na wachezaji wanakaa vizuri pale, wanajiangalia vizuri. Halafu wale wa KBC wakaitowa ile picha pale, vile picha vikawa havionekani. Sasa mtangazaji mmoja akamwambia Ali Manga, haya maneneo unayoyasema hapa, watu wote wanaona. Watu wanapigana pale unasema referee anangoja kipenga, namnagani? Kwa hivyo sasa ni directives zile zinatoka kwamba hatutaki fujo, useme hakuna fujo.

Swala la nominated MPs, wasichaguliwe na Rais, sisi tumesema nominated MPs hawata chaguliwa na Rais. Lakini tumesema kuna wabunge ambao watateuliwa kulingana na nguvu ya vyama ambazo zimepata kura katika bunge. Hili Bunge tulisema ni ya wale wabunge 210, kwa Kinango, wa Matuga, wa Msambweni, wa Likoni, wa Kaloleni, wale watachaguliwa kama kawaida. Halafu, vile vyama ambavyo vimepata nafasi ya viti vingi kule Bunge, tumeipatia nafasi za mixed proportion. Utakaye utatuwa Mbunge wako, chama kitateuwa wabunge wake maalum kulingana na viti, nguvu ya vitu walivyonavyo kule Bunge. Tuemsema hawa wabunge wawe ni 90, watu wengine wamesema hao ni wengi mno, wengine wanasema wanasema wanatosha, mko na uhuru wa kusema. Kwa hivyo wale watakuwa ni mia ngapi? Ni mia 300, wale wa-Bunge wa lile Bunge la kawaida. Wale 90 tumesema iwe ni mix, mume, mke. Kwa mfano, kama Shirikisho wamepeleka wabunge 20, katika 210, kwa mfano, sasa Shirikisho itapewa let say iambiwe chagueni wabunge saba, nyinyi wenyewe kama chama mtuletee. Lakini saba wale lazima wa kwanza ni mume, wa pili ni mke. Wa tatu ni mwana mume, wa tatu ni mwanamke, kwa hivyo utapata wanne wanaume, watatu kinamama, ndiyo tunaita mixed proportion. Kila chama ambacho kimepata viti katika Bunge. Kwa hivy si kazi ya Rais tena, ni kazi ya vyama vyenye ambao watachagua. Nimesema tayari watu wamesema hao ni wengi sana wapunguzwe, tume kubali.

Halafu mkaeleza habari ya Chief, mumesema machifu wawe wamechaguliwa na wnanachi. Kwanza tumesema kwamba ma chifu kwaza hawapo. Lile swala la kwamba wachaguliwe na wanachi au ule limeshaondoka; tumesema hawapo, Sub-Chief hawapo, D.O. hapao, DC hayuko, PC hayuko. Sasa imebakia sasa zile serikali ambao itazichagua, zitafanya kazi zote, za Chifu, na za Councillor, inafanywa pamoja, kazi ya DC, na ya DO inafanywa na District Council. Kwa hivyo ni kama kusema mtawachagua wenyewe, maanake tutaanza serikali ya Kijiji, tutawachagua au tutawateua sisi wenyewe. Wale ndio watafanyia kazi zote wenyewe, wale ndiyo wanafanya kazi zote zile. Kwa hio, wale walikuwa wakisema tunataka wazee sijui walipwe mshahara, automatically sasa wakisha chaguliwa wako kazini hawa, mishahara yao tayari iko ndani. Lakini sasa ni wale wananchi wenyewe, wataamua kama hapa tumewekwa wazi. Kama ni uchaguzi mtaamua wenyewe, pale kwenye kijiji chetu. Kama ni uteuzi, mtaamua wenyewe pale kwenye kijiji chenu. Lakini hawa wote wataata mshahara. Tumeelewana hapo?

**Chorus:** Ndiyo.

**Com. Swazuri:** Halafu na nimesema hao ni baina ya 6 na 10. Najua watu wengi wanataka wale wengi, kumi. Katika wale wako 10, ambao mumewachagua, au mue teua hawa wale tutawachukua wawili pale ndiyo wataenda wataunda serikali ya Location. Lakini mkubwa wa Location atachaguliwa na wananchi wote wa Location. Atakuwa na debe lake. Huyo ni mkubwa wa location. Sasa yule mkubwa wa location yule, yeye anachanganya kazi zote mbili, administrative na legislative. Administrative ni kazi ya Chief, legislative ni kazi ya Councellor, zogte amepewa yeye. Ndiyo maana tukasema kura iwe ya siri, asijue alichaguliwe na nani, wala alikataliwa na nani kwa mlolongo. Sasa atakuwa yeye ana haki ya kufanya Chief anavyo fanya, na haki ya kufanya Councillor anavyo fanya.

Halafu tukasema kuna Bunge sasa la Wilaya, Bunge la wilaya litachaguliwa directly, yaani wananchi wenyewe mtachagua moja kwa moja. Wanaotaka kupigania viti vya wilaya watajitangaza wenyewe, wafanye compaign wenyewe, mimi natoka

Mwavumbo, mimi natoka Kinango, lakini nimeenda kufanya compain Lunga Lunga au Ng'ombeni, nataka Mbunge wenzeni wa serikali ya wilaya, 30, hao tutawachagua sisi wenyewe. Mikubwa wao ni District Governor, na atakuwa na debe lake tofauti. Sio hawa 30 wachaguliwe halafu hawa wakachague mkubwa wao, a,a. Tumesema sasa yule mkubwa atachagua mbali hata hawajui nani wanawapigania vile vite, lakini yeye mwenyewe anasema mimi nintaka kuwa mkubwa wa kwale, yeye apigania kiti chake. Hizo ndizo serikali tumesema haitachaguliwa namna hio. Kwa hivyo uhuru ni wenu.

Nyinyi wakaazi wa Kwale mkisema huyu hatufai anatolewa mnachagua mwingine. Upande wa ndovi, ukiangalia sehemu ya 241 tumeandika. Upande wa ndovu na wanyama wote kwamba sasa compensation yaani ile ridhaa ni lazima, na tumesema kwamba pia upande wa wanyama utaona ni Serikali ya Location na Serikali ya Wilaya ndiyo ambazo zitaangalia masilahi ya misitu, mbuga za wanayma, na kadhalika. Kwa hio kuna ushirikiano sheria pale imetoa wamawasiliano baina ya wenyeji na KWS na ile Tume ya National Environments Management. Halafu ukasema Mzee Mwabaya kwamba hukuona Serikali za Majimbo, nimesema Serikali za Majimbo ziko. Kuna Serikali ya Kijiji, Serikali ya Mtaa, Serikali ya Wilaya, na kubwa kabisa ni Serikali ya Majimbo. Hatukuandika neno Majimbo maanake tumesema limepakwa matope, watu wanalelewa vibaya, au wanataka tuelewe vibaya, wanafikiri tunataka kufuza wengine, dnio maana hata haikuliandika. Tumeandika Provincial Council badala ya kusema Majimbo. Lakini ni hilo hilo.

Baraza la Wazee kuhusu sheria nimsema kwamba kuna traditional courts, iko hiyo. Wazee watakaa pale traditional courts, wata amua cases zile nimesema za kinyumbani zile. Environmental Protection, pale watu wana miti wanataka kukata, hiyo imelezwa katika Serikali za Wilaya, na Serikali Kijiji zina mamlaka. Watahakikisha kwamba ule mti unataka kuukata utadhuru mazingira au la, tumeandika katika section 239. Kwa hivyo yaka kama unataka kukata sasa utawaasiliana na Serikali ilio karibu kabisa ile ya Kijiji au ya Location.

Bwana Mwero umeeleza kwamba unataka National School katika kila province na University, hiyo ni sawa. Kwanza sasa Serikali za Majimbo sasa ndiyo zitakuwa zinafanya haya mambo. Wakishindwa washindwe hao wenyewe. Lakini mamlaka, education services ni kazi yao sasa. Wapiganie vile ambavyo wantaka wawe na university. Hiyo wame pewa sasa, mamlaka ya kufanya hivyo.

Pombe ya mnazi**, (interjection)** ----- si pombe ya mnazi?

**Majibu:** Hapana--------

**Com. Swazuru:** Ah okay. Basi nitazungumzia yote mawili. Pombe ya mnazi, manaake Ganze, Kaloleni tuliulizwa kuhusu pombe ya mnazi. Na hata hapa watu wame sema pombe ya mnazi. ------- sasa tuanze na pombe ya mnazi. Pombe ya mnazi ukiangalia jina lake halipo kwenye Katiba. Sasa nimewaelezea pale mwanzo kwanza tunamambo ambayo tulisema tutayaweka katika Katiba yanaonekana wazi. Kuna mambo mengine tutaandika mrundo wa mambo ambayo yabadilishe katika sheria

zilizoko. Pombe ya mnazi imeingia hapo. Si pombe ya mnazi pekeyake, tuna pombe ya busaa, Kakamega, Kisii, walisema ni lazima, tuna pombe ya Muratina, Central Province, Meru, Embu walisema ni lazima iingie, kuna tembo inatwa Denge, Wataita wakasema ni lazima iingie hapo. Sasa hatukukataa tukasema kwamba sasa sheria itairuhusu tutaihashidisha ili mambo yao yaingie hapa.

Mnazi, kuna malalamiko kwamba mnazi imedharauliwa. Mkorosho umedharauliwa, manaake ni mazao ya Pwani, au sio hivyo. Kwanini kahawa iwe na bei ya juu ilihali Manzi na ndiyo kitu inatumika kilasiku. Mnazi hauna hasara yoyote, kutoka kuti mpaka lile ganda lake naye yote yanatumika. Sasa kuondoa tatizo letu tumesema Serikali ya Majimbo, Serikali ya Wilaya ya Pwani nio itafanya kazi. Kabisa tumetoa expressly pale. hawa ndio wanajikumu sasa kama nazi zikikosa bei tusilaumu Serikali ya Nairobi tena. Kama Korosho matapewa Korosho haukuinuka au Korosho zimekosa bei sasa si lawama ya Serikali ya Nairobi, kwa sababu Serikali hii Wilaya zimepewa mamlaka sasa, ku hakikisha kwamba mazao yao yanauzwa, kuhakikisha kwamba wananchi wao wanafaidika na mazao yao.

Disabled wale wenye vilema, Bwana Joseph wameeleza pale, ukiangalia section 39 nafikiri 39, utakuta kwamba hayo anasema Bwana Joseph, yote tumeyaandika pale kama nitakusomea kwa ufuupi kwamba wananchi wale ambao wana vilema wanatakikana wa-enjoy all rights and freedoms. Unasikia? And to participate as fully as they are able in the society. Wahusike kabisa wanavyo weza, kama wanataka kuwa Board Governor achaguliwe asichaguliwe ana haki ya kufanya hivyo. Kama ni Chairman sijui wa nini, anna haki ya kufanya hivyo. Tukasema kwamba Serikali na sheria, na policies zita hakikisha kwamba haki za wale wenyw vilema, kama binadamu zinalindwa. Hiyo tumeandika. Ielimishe wananchi kuhusu hali za hawa wasiojiweza, and need for respect, wapewe heshima yao kama binadamu, tumeandika hiyo. Tukasema wahakikishe kwamba education, yaani elimu sehemu zinazo fundisha, zinazotoa elimu na facilities za disabled persons zinapatikana katika jamii zote. Halafa ensure access, uwezekano ya kwamba kilema anaweza kufijka kwenya public transport, all places, sehemu zote majumba hayo, na information and communication, including Braille and sign language. Kuna mtu yuazungumza? Unasema nini, sikuelewi, hebu inuka useme vizuri, si kuelewi mimi……….

Haya nimekusikia. Watu kumi wengine. Wakwanza chairman, wa pili ni nani, wale ambao wanataka, eh, mzee wangu wewe ni number mbili, number tatu ni nani, yule nyuma pale, mama ni number nne, number tano ni ule mzee, number sita, ahh tuchukue hawa kwanza. Number moja, number saba Bwana Mng’ong’o hapa.

**Desmond Kitainge**: Mimi ninitwa Desmond Kitainge, na nikinshukuru sana kwa Commission hii kwa sabu ya kazi ambao imefanya. Kitu ambacho nimeaangalia na ninitaka nieleze zaidi ni kwanda, tulisema hii Constitution ni sheria tumetunga. Na sheria ikitungwa:

(a) Lazima iwe ina part yake ya pili. Kwa mfano ikivunjwa itafanywa aje? Constitution yetu au Katiba yetu ninona iko wazi. Kwa mfano tunasema elimu ya msingi iwe ya lazima. Jee kama hawa wanao hitaji wachukue jukumu hilo hawakuchukuliwa?

**Com. Swazuri:** (In audible)

**Desmond**: Ndiyo nilikuwa nataka kujua, kwa sababu iko wazi sana.

**Com. Swazuri:** Tumeleza enforcement and Defense of the Constitution. Watau wamelalamika kwamba wanasikia elimu ni ya bure lakini kuna malipa, sijui nini, sasa ni bure jina tu lakini twalipa, sasa hatujui namna gani. Tukiangalia kifungo cha tatu, tumeandika kwamba, mtu yoyote anaeza kushtaki on the ground that anything contained in this Draft, iko hapo.

**Gerald Machare:** Mimi ni Bwana Gerald machare. Yangu ni shukrani kwa Tume hii, kwa kazi iliopewa na ikaturidushia leo kuja kutujulisha mahali wamefikia.

Pili nimesikia Tume hii au kwanye matangazo wakizungmuza kwamba leo Tume hii itakuwa na kikao hiki. Ikazungmuza kwamba unahaki ya kutengua ama kutoa shukuruni ama kuongeza. Hapa kuna kitutulicho sikia tukisema kwamba Tume hii imeamua uchaguzi uwe wa siri, uwe kwenye debe. Hivyo ndiyo nilivyo elewa ama si hivyo. Je ikiwa leo hii ano husika atatutisha kama anavyotaka, kama hivi sasa hivi alivyo kosa vyama vingine, na hata hivyo uchaguzi wa Rais umefika. Utakuwepo ukweli pale? Ikiwa Katiba hii inafanya kazi, samahani kwa nyinyi, nyongeza?

**Com. Swazuri:** Haya.

**Gerald Machare**: Je ikiwa Katiba hii inafanya kazi, je hivi sasa wananchi hawataweza kuisimamisha mpaka kura hadi Katiba mpya hii tutaipata?

**Ali Juma Nyae**: Asante sana, kunipa nafasi hii, niweze kuuliza maswali mawili. Kwa jina ninitwa Ali Juma Nyae. Swali langu la kwanza. Umesema kwamba Provincial Administration Katiba mpya punde itakapo tumika itakuwa hakuna Provincial Administration. Sasa swali langu nauliza, je hii Katiba mpya ikitumika wao wataendela na kazi ama itakuwa ni basi, wataenda kwa msururu wa uchaguzi?

Swali la pili, nimesikia katika vyombo vya habari kwamba Mwenye Kiti wa Katiba Bwana Professor Yash Pal Ghai kwamba Katiba itakuwa tayari mwezi kumi na mbili, tarehe kumi na mbili, waakati tutako sherekea sikukuu ya Jamhuri. Je swali langu lasema hivi, inainawezekana huende kwenye uchaguzi kwa kutuma hii Katiba mpya? Asante.

**Gladys Tatu:** Nami kwa jina naitwa mama Gladys Tatu Nzozo, nikiongezea ama nikirudi upande wa elimu, nina kuta kwamba hapa kwetu Kinango bado kuna shida, kwanza zaidi kama vile tumesema elimu itakuwa ya bure kwa shule ya mshingi. Ikiwa ya bure kwa shule ya msingi, haitakuwa mwisho wa shule ama wa masomo kwa watoto wetlu. Tutakuwa tumeendelea tena na kidato cha kwanza na kuendelea. Hivyo, nikimaanisha kwamba sisi wazazi, hatuna nguvu moja. Wazazi wako tofauti, wazazi

wako na nguvu tofauti, wengine wanajiweza, na wengi hawajiwezi. Wanapofikia kidato cha kwanza mpka cha nne, kuna kushindwa ama kuweza. Walewanaoshindwa ni wale wasiojiweza. Na hapo hua kuna hii pesa inayoitwa ya bursary ambayo sisi sisi wazasi tusiojiweza tunaitwa tunachanga changa zile pesa za bursary ili tusaidie wale ambao wako chini zaidi walioshindwa kabisa. Hiyo pesa kusema ukweli hua inaenda kwa wale watu ambao wako juu yetu, ambao wanajiweza, watotot wao wanaendelea, wetu wanabaki pale chini.

Hivyo nilikuwa ninasema kama kutateuliwa tume fulani ambao itaangalia yale masiliahi, ili watoto wetu wasikome darasa la nane, waendelee wamalize hasa watoto wa wale wazazi ambao hawajiwezi, nao wamalize form four. Na pia wanapomaliza form four, kuna kuenda college. Yule yule mzazi aliyeshindwa na mtoto kumpeleka form four mpaka akasoma na bursary ama akasoma na mchango na ni msaada fulani fulani huku na kule atashindwa pia na college. Akishindwa na college, Serikali yetu imeshindwa na kuajiri watotto ambao hawajakuwa na ujuzi ya aina yeyote ile.

Tutabaki na ule umaskini tuliokuwa nao kutoka pale mwanzo, ambao watotot wetlu wameshindwa kwenda college, hakuna kazi tunaendelea kukaa nao pale majumbani. Hivyo nilikuwa ninasema kama itawezekana Serikali yetu na Tume yetu ya uchaguzi kabla ya kongamano, tuangaliliwe vile tutakayotunzaweza tunaposhindwa na kupeleka watoto college, ama kama tutaweza ile nusu fees za kwanza, ya pili na ya tatu, tuataweza kusaidika vipi ile yule mtoto aendelee na ule ujuzi ili aje pate kazi kwa wakati unao faa ili zile shide zisiendelee na umaskini katika Kenya yetu uzidi kuwa pale pale. Asante

**Mwauchi Muruche**: Kwa jina ni Mwauchi Muruche. Mimi kwangu ni kuuliza ni kuongezea hiyo swala ambalo tulikuwa tumezungmuza mbeleni. Urithi wa wanawake, kama umeondoka, amefariki, au mwanamke amboye umemzaa ni mtoto wako anaweza kurithi ule urithi wako au ni mume peke yake? Kwa hivyo mimi nikuuliza. Nimekuja kuchelewa ninfikiri lakini sikusikia jambo likitajwa, habari ya urithi kutoka wanawake. Asante.

**Mwaperu Mwandao**: Kwa jina mimi naitwa Mwaperu Mwandaro kutoka Puma. Kwanza nikushukur Tume kwa kusanya wakio kusanya ya wananchi wote, lakini swali langu liko hapa na liko ngazi za juu sana. Mawaziri watateuliwa na Wabunge. Wale watakao simamia katika kama ma manager pia ni Wabunge. Je, ile kabila ambalo likuwa ni dogodogo linatafutwa usawa uliangalia sana makona usawa kweli utatendeka, kwa sababu ikiwa WaBunge ndio watakao teuliwa hawa watu, jina la Mwaperu kule halitapendekezwa na Wabunge wa Kikuyu. Na watakuwa wengi kwa sababu wao huko ni Wakikuyu, na hata katika hizi sehemu zetu pia wameingia, na itakuwa ni kura. Je sisi kweli nafasi hio tutapata? Kwa hivyo Tume iangalie zaidi kwamba usawa utendeke. Vile vile pia, nikiongezea katika mambo ya utawala kwamba sasa utakuwa ni tuchague watu kumi ama sita, ndiyo mmoja mwengine pale awe ni mkubwa. Hawa wote watapata mshahara ama itakuwa ni yule mkubwa peke yake? Hawa watu ambao tutawachagua katika Kijiji, kwa sababu tutakuwa tumevunja mambo ya Assistant Chiefs, ma Chiefs, kwa hiyo ni ile Tume ambayo tutakuwa tumeiunda. Hawa wote watapata mshahara ama itakuwa na yule mkubwa peke yake. Hayo ndio yalikuwa ni maswali yangu.

**George Mng'ong'o**: Kwa majina mimi naitwa George Demu Mgno'ng'o., natoka huko upande wa Mazeras, na kwanza ningependa kumuunga mkono Bwana Kasisi, tunatoa pongezi kwa Commissioner Swazuri kwa vile anaweza kueleka vyema. Ile kazi iliopita ni kubwa tunatumae kuna wengi ambo peke yetu tukijariubu kusome haya mambo hatukuweza kuvuka ile mpaka ambao imo kwenye haya maneneo lakini Bwana Commissoner ameweza kueleweka vyema.

La pili ningependa kusema kwamba tuombe ya kwamba hii Katiba ikamilishwe kwa mapema iwezekanavyo ili ile Serikali ile tunaiomba kwa Majimbo iweze kuleta haki zaidi mikononi mwa wananchi, kwa sabau hayo ndiyo maobi yetu. Sisi kama watu wa Duruma au watu Wadigo, tunatumae kati ya maswali yaliolizwa ka Bunge toka mwaka 63, yameulizwa yale yale, maiaka mitano baada ya mitano, baada ya mitono. Na suluisho haliljafika. Lakini lile lengo ambalo linaoneka katika hi Katiba mpya zaidi kama tutakuwa na lule mabadiliko ya kwamba Serikali itakuwa iko mikononi mwetu. Sasa ni sisi tutaangalia kama kuna cooperatives za mikanju, kuna cooeratives za minazi, an vile ambazo vitapatikana katika mashamba yetu tuhakikishe tumepata bei nzuri katika soko na tuweze kuleta maendeleo zaidi kwenye areas szetu. Kwa sababu Bwana Commissioner vile ambavyo twamuelewa, amepata usome wa kutosha, si hivyo? Lakini hata yeye tukamuwache pekee yake, yale maendeleo hatutapata. Kwa sababu kuna wengi wameenda mbele hii miaka minigne, na maendeleo mpaka sasa yatali na matatizo. Lakini katika Katiba mpya, tuna hakikisho ya kwamba zile nguzo za kuteremsha mendeleo katika kila sehemu zitakuwapo. Asanteni.

**Peter Kilawa**: Kwa majina naitwa Peter kilawa, mkaazi wa hapa Kinango. Ninge anza kwanza kwa kueleza shangaa wangu na huzuni kwa ajili ya malipo yale yamepatiwa hii Tume baada ya kufanya kazi hii nzuri tunavyoiona.

Jambo la pili nina swali nimesikia kwamba tutateua Wazee wa Vijiji na kupitia pia ngazi ya Location, tutateua watu lakini ningependa kupata zile sifa ambazo hawa watu wanastahili kuwa nazo. Kwa mfano kama yule ambaye atachaguliwa kuisimamia Locationos, numesikia atajumuisha pia kazi za Chief, ningependa sana kufahamu zile sifa ambazo yule mtu anastahili kuwa nazo. Lingine ni kwamba maWaziri, watateuliwa na Bunge, na ni lazima hawa wameelimika katika maswala yanaohusu ile wizara ambao wata simamia. Ninapenda kujua kwamba ni mambo gani yatazingatiwa katika kuteua wale Mawaziri, kwa sababu wako watu wengi wameelimika. Kunaweza kuwe watu kuma wameelimika katika nyanja za Wizara ya Utalii, ama watu kumi wameelimika katika nyanja za Wizara ya Elimu, je, itazingatiwa mambo gani katika kuteua wale watu?

Na la tatu, ningependa ku fahamu hawa wazee tutakao chagua katika ngazi za vijiji location, na kuendelea, je watahudumu kwa kipindi cha muda gani, au wata hudumu hadi wastaafu wakiwa an umri gani? Asante.

**Kilaala Madaka**: Kwa jina naitwa Kilala Madaka, natoka huko Pumo Location. Yangu ni kama wenzangu walivyo kuwa wanachagnia kwamba kutoa shukurani katika Tume hii ya Katiba. Wamefanya kazi nzuri sana kwa sababu wameaandika yale yetu ambayo tumeyatoa. Lakini labda mimi pekee yangu sikusikia, maana unaweza ukatoka nje ki akili. Hii sheria ambayo tumeitunga ambao imesomwa pale kwa Serikali zijayo, vile itakayokuwa inaendeleza. Kuna mahali sikusikia, hii sheria ile tuliitungaghafla, mimi ninaweza kusema hivyo kwa sabaqbu hatukuelemishwa, ili tukaelimika sana, tukaanza kuja hapa tukaanza

kutoa yale maneno. Je sheria ile tume---- mwananchi ije imkalie ngumu kwa sababu ameelewa na msimamo wa sheria. Ina miaka mingapi ili tuweze kusikalia pale ambapo tumeona ni sawa turekebishe? Hilo swali langu liklokuwa ni hilo tu.

**Nyawa Ngana:** Kwa jina langu naitwa Nyawa Ngana kutoka Puma. Mimi nilikuwa nataka kuulizia jambo moja. Jambo lenewe ni hawa wenye kuchukua makandarasi either Nyumba ama barabara, kitu kama hivyo. Sasa kusema kweli, hawa wenye kuchkua kandarasi za shughuli hizo kama kufanya barabara, mwengine huwa anachukua kandarasi vizuri, anamaliza. Wengine kukwamia katikati, ama wengine hua hawafanyi kabisa. Sasa kulingana na sheria ama kulingana na hii Katiba yetyu ambao tunarekebisha, watu kama wale ambao hua wanafanya kazi zao ovyo ovyo, hii Katiba iseme kama wale hua wanafanyiwa nini, mpaka mwisho wawe tumekomesha watu kama wale. Maanake sass itakuwa ni vigumu, ama itakuwa ni vigumu kwa Serikali. Serikali imetoa kandarsi ifanwe Barbara kutoka hapa mpaka Mariakani, lakini ukute barabara hiyo badala itengenezwe imeharibiwa. Je Serikali huwa inachukua jukumu gani, na hasa kwa Katiba? Asante.

**Henry Ziro:** Majina yangu ni Henry Mzomba Waziro, natoka sehemu ya Taru, na mimi ni mmoja wale providers niklikuwa hapa Kingango. Swali langu ni moja na linahusu matatizo mawili. Matatizo ya wa Kenya ya kwanza ni ukosefu wa kai, ya pili kuzorota kwa uchumi. Je Katiba ambao tunanuia kuwa naye inaeleza vipi matatizo hayo mawili? Hapo tu. Asanteni.

**Joseph Rumba Kagena**: Kwa majina naitwa Joseph Kagena Kutoka Location ya Mtaa. Mimi swali langu ni moja. Tukiangalia hali ya uchumi, hasa sehemu hii yetu ya Kinango, iko chini sana. Matatizo makubwa ni kwamba sisi wananchi hatuna fedha za kutosha, za kuweza kuendeleza mambo yetu ya kilimo, ujapokuwa inasemekana kwamba kilimo bado kinasajiliwa huko, lakini ninaomba Katiba hii mpya ambao inaendelea pia sisi wananchi wa kawaida tuangaliwe kidogo tuwe tunaweza kupata hizi fedha, pia masharti yake yasiwe magumu sana, na ile riba pia inayotozwa katika fedha hizi iwe hali ya mwananchi wa kawaida kuweza kulipa kwa wakati mzuri. Hayo ndio maoni yangu. Asateni.

**Com. Swazuri:** Kwanza kuna swali sikulijibu wakati ule ulipoulizwa. Swala la Mawaziri kutoka nje ya Bunge. Kuna mtu ameuliza swala hilo. Tunasema kwamba ltutachagua Wabunge, halafu wakifika kule watachagua maWaziri, ambao hawatakuwa Wabunge, sababu tumeona kwamba Mbunge akiwa pia ni Waziri either afanye kazi vizuri kama Waziri wa taifa nzima halafu watu wake wapate tabu, au aamue kutumia ofisi ile ya Waziri kufanyia watu wa sehemu yake. Kwa hivyo kuondoa hiyo tashishi hiyo ndiyo tunasema either wewe uwe Mbunge kabisa kabisa, au uwe Waziri kabisa kabisa. Hiyo ndio sababu ya kuwa-separate hawa Mawaziri, wa-Bunge wasiwe na kazi mbili; manake safari hii tumesema kazi ya Wabunge ni nyingi na tumeiandikika. Kwa vile ambavyo wako accountable to the peoples: sasa, anaweza kukwepa kama ni Waziri aseme kwamba mimi unajua nina kazi nying bwana kule Nairobi sasa haya mambo mengine msiniambie. Itakuwa bado yeye amekwepa. Lakini hapa tumemuandikia kazi zake kama Mbunge, tuna-tick akifanya tuna-tick right, akikosea basi, sasa tunajua hapo huyu hakufanya kazi.

Tukasema kwamba ofisi zote ya Kenya madaraka yote ya Kenya ni lazima yagawanywe kimikoa. Ni broad principle katika.

Ni lazima wagawanywe ki Mikoa. Kwa hivyo kama waziri tumesema watakuwa 15, wizara ni 15 pekee yakee. Mawaziri ni waziri mmoja mmoja, ka kila wizara, naibu wa waziri pia ni mmoja mmoja kila wizara. Na tumesema hawa wagawanywe equally to the Provinces. Hiyo ndiyo principle yetu. Tumesema kwamba lazima ofisi zote za ki taifa zitazingatia misingi ya kimukoa kwanza muhimu zaidi pamoja na DC, na kadhalika, lakini kwanza mjue wizara zote zimetoka mkoa moja. Kwa hio hilo liko hapa, tutawagawanya, kila mkoa watapata watu wake.

Halafu upande wa uchaguzi utakuwa naweza tumika na Katiba mpya au vipi? Hilo swala tumeuliswa kila mahali na hua talijibu tukisema kama Tume tumekuta kwamba utakuwa ni ubora zaidi ikiwa uchaguzi utakao kuja utafanywa Katiba hii mpya, hayo ndio maoni yetu. Ndiyo maana tukaharakisha. Kuharakisha ili tumalize ili wananchi waende kwwenye uchaguzi kutumia Katiba hii mpya. Ikiwa itakuwa tayari mwezi wa kumi na mbili tumesema kwamba kunatakikana kama mwezi moja au mwezi miwili kutengeneza hizo ofisi ambazo tumeziunda upya. Kwa hio tunasema kwamba, angalao ltupatiwe kama miezi miwili au moja japo baada ile tarerhe 12 kuhakikisha kwamba kila kitu kimewekwa sawa. Wale watakao chaguliwa mpya, zilve ofisi mypa tuwe tumeziunda vyema. Lakini hata tunataka uchaguzi ufanywe na Katiba mpya. Lakini sasa uwezo huo hatunao sisi. Sisi tuliambiwa tuandike Katiba, hatukuambiwa tufanye uchguzi. Uchaguzi ni baina ya wananchi na wale wana siasa walioko pale, hayo ni maelewano na sisi Tume hatuambiwa tuandika Katiba ya uchaguzi, tuliambiwa tuandika Katiba, and tumeandika, lakini tungependelea mambo haya tuanze sikui mpya, na mambo mapya, huo ndio msimao wetu.

Je wale wafanya kazi wa Provincial Adminsitration watakuweko au vipi? Tumeshasema kwamba hawa ikiwa Katiba mpya itaanza itawapa miezi mitatu ya ku-handover. Tumepewa 90 days pale, kwa sababu uwezi kukata leo halafu kesho ukaanza nyingine, haiwezekani, tunajua hivyo. Tuna siri nyingi za Location wanazojua Chief, and sub-Chief. Ukimfukuza leo file zingine atakwenda nazo atasema watajua wenyewe, si wao werevu. Ah tuangalie. Aa, miezi mitatu, maji yanao ingia yanakutana na maji yanayo toka. Baada ya miezi mitatu tunaandika hapa kwamba officers vote wa Provincial Administration watarudi kwa Office of the President, itajuwa itawapeleka wapi. Lakini sisi tulichagua wetu hapa.

Elimu mama ameeleza pale, tumesema ni kama, ukiangalia vizuri kabisa mama ni kama tuna rudisha zile sehemu za zamani, tunarudisha yale mambo ya zamani. Kwa kweli ukiaangali ni kama tunarudisha Katiba ya Lancaster, ambapo elimu ilikuwa inatolewa na nani, Districts, County Council ndiyo ilikuwa inatoa elimu na kila kitu. Tumerudisha hiyo, lakini unakumbuka mama hata secondary schools tulikuwa tukitoa fees. Lakini primary ndio ilikuwa ni bure, secondary tulikuwa tukitoa, hata mimi ninkumbuka mimi babaangu alilipa fees. Tumesema kwamba ziwe na fees.

Na bursary scholarships sasa ni kazi ya Serikali kuu, na Serikali ya Majimbo na Serikali ya Wilaya. Watu wengi hapa tulisome na bursary, zilizo zikifanyiwa hapa pale County Council. Tume rudisha hiyo hiyo sasa.

**Swali**: (Inaudible)

**Com. Swazuri:** Tunasema ndiyo hiyo hiyo tunasema kwamba. Kuna corruption wale ambao wanatakikana kupewa hawapati. Hio hatuwezi kuandika kwenye Katiba lakini tunasema tu kwamba unaujua utaa wako, tajiri unajua, maskini mnajua. Ikiwa unakuta kwamba burseries zimetoka zimepewa mtoto wa millionaire Katiba yote inakupa uhuru ya kwanda kulalamika, yote, vifungo vyote tuliangalia. Hata kushtaki ile Serikali ya District, unaweza sasa. Umesikia mama, hata ile Serikali ya District kwenda kuishtaki kwamba mumefanya makosa mumepewas kifungo hapa, wawweza. Na kama itaendelea hivyo basi nyinyi mnaandika tu District Governor amefanya hivi, la kwanza, la pili, la tatu, nje. Kwa hivyo uhuru umerudishwa kwa hawa wananchi wenyewe.

Na upande wa employment mambo ya vijana hawapati kazi, ukiaangalia hapa tumesema kazi ya kuandika watu itakuwa ni ya Districts, Majimbo. Hawa ndio watakuwa na kazi ya kuandika, hata police pia tumeandika, wao ndio watawaandika, wale police wa local, wao wataandikwa na District and province. Sasa ni sisi wenyewe tunyimane kazi au tupatiane kazi, sisi wenyewe. Uridhi wa akina mama, tumeandikwa kwamba kwana haki za akina mama ni lazima zipatikane. Usitumie mila kudhulumu mama. Kwasabu wengi Wazee wengine hua wanatumia mila, ikawa inafaa, wanasema hiyo ni nzuri. Ikiwa haifai anasema mimi ninruka kwa dini. Tumesema za akina mama zitolewe peupe. Mtoto wakishchana amezaliwa pale nyumbani. Kwao ni wapi yeye?

**Chorus:** Ni hapo.

**Com. Swazuri:** Kama ataamua na siku hizi wanafanya hio kazi hiyo, wataamua kwamba hataolewa, au ataolewa ataachika halafu arudi nyumbani. Sasa babaake ni nani? Ni wewe. Sasa mtoto wako utamnyima aende wapi? Eh wazede? Hebu tuangalieni hapo. Umemzaa mwenyewe yule, akiolewa akienda akikaa huko sasa hiyo file yake tumeondoa hapo, yeye mambo yake yote yako kule. Lakini kama ataenda mambo yaharibike baada ya miaka 10, akija hapo huwezi kummwambia mwanangu ulisha ondoka mimi si babaako tena aa. Ni mtoto wako wanaarithi wapi kwa baba yao. Lakini yule mtoto wake anarudi wapi? Kwa babaake. Tumesema kwamba tusiingilie maswali ya wanawake. Tukasema swala hilo tutatatuliwa kwa mila, na mila tunazijua ni hivyo. Na dini, kuna dini kama ya Waislamu ambao mali ya mwanamke hata akiolewa ulaya, ya babake tayari share yake iko. Hata akirudi, asipo rudi lakini babaake akifariki share yake tayari iko. Anaambiwa pana Nyumba yako hapa sasa angalia mwenyewe, sis tushachukua zetu. Kwa hivyo ltumesema dini na mila. Kitu ambacho hatutaki ni kufanya mambo kwa sababu yana tufaa sisi yanao dhuru wengine tukasema hilo ndilo nzuri, ku kwepa kwepa. Huku ni nzuri, huku si nzjuri, huku ni nzuri, a a! Usawa kila mtu apate haki yake. Mawaziri nimesema kwamba tutaangalia wanatoka sehemu zote.

Halafu, je wale waze tutawachagua watapata--- kwanza nataka kuwajulisha kwamba ile Serikali ya vijiji sio Serikali ya Wazee. Hatukusema ni ya wazee, tulisema ni Serikali ya kijiji. Wananchi wenyewe wajue kile watafanya uamuzi. Kama watasema tunataka kura yeyote anaweza kugombania. Kijana, mzee, mama nani, kila mtu, kura ndiyo itaamua. Au wenyewe mtasema aa, sisi tunataka Mzee Desmond ndiye anafaa, Mzee Nguche anafaa, ama Gladys anafaa, nyinyi wenyewe lakini. Uhuru ni wa wananchi wenyewe kuamua. Kwa si wazee. Sheria hapa haikusema wawe ni wazee wa miaka 50, aa, yoyote kwenye

Serikali, akizidi miaka ishirin na moja, huyo anafaa kuchaguliwa au kuteuliwa. Kwa hivyo wale mishahara yao tayari iko, nishaeleeza hio, watapata wote mishahara, iko kwa Serikali itatoa mishahara. George ninafikiri umeeleza vizuri sana Bwana George habari ya Majimbo na mimi nantilia mkazo, mlikuwa mnataka na tumeyapata, sasa ni utekelezaji ndio ambao unatakikana.

Qualifications hio ni kwela nimeeleza pale mwanzo, hiyo nafikiri hatukuiandika, sifa za wale wana vijiji, na hata wale wa District, hatukuandika. Kwanza hawa Wazee wata-serve kwa miaka mingapi? Na hii Serikali ya Kijiji, tumesema hii Serikali zote ya Kijiji ya Wilaya, ya Location ya Majimbo, miaka mitano mitano. Miaka mingapi, mitano, sawa sawa na Wabunge. Lakini National Council, in Upper House, lile Bunge la wakilishi wale mia moja niliwasema, wale watachaguliwa kila miaka minne. National Council, lile Bunge la waze lile la kitaifa na kila district, tumesema Wilaya hi ya Kwale, mmoja Kilifi, mmoja Malindi, mmoja akina mama wanne kutoka kila mkoa, wale watu miamoja, wale watachaguliwa baada ya miaka minne. Tumefanya ile makusudi kwa sababu isiwe Bunge likivunjwa hakuna Serikali. Sasa wale wengine wakiwa ni miaka minne kwa amfano ltukichagua mwaka huu tusema kuanzia January iwe tuna Serikali hizo, National Council iko. Hawa Wabunge wa kawaida, wa Lower House watafanya kazi kwa miaka mitano. Lakini hawa wengine watafanya kazi miaka minne. Miaka minne ni 2007. 2007 tunafanya uchaguzi wa National Council. Wale wabunge wa kawaida bado wana mwaka mzima. Tuna chagua hawa halafu ule mwaka wa 2008 ukifika Bunge likivunjwa bado tuna Wabunge wale wa National Council, hakuna vacuum, ndiyo maana tukaweka namna hiyo. Kwa hivyo wale Wabunge wa chini au serikal za chini ni miaka mitano.

Tutarekebisha Katiba baada ya miaka mingapi? Kwanza tumesema sababu ya wananchi kutoa maoni yao ni hakikisha haya marekebisho hayawi ya ovyo ovyo, ndiyo maana tukachukua muda mrefu, miaka miwili kusikiliza na kuenda kufanya corrections ili tukitoka hapa tukianza ile race, basi, tuwe tunaanza. Lakini haiwazuii wananchi kufanya marekebisho. Vifunguo vyote hapa tunawapatia nafasi. Ikiwa mnakuta kwamba wananchi kuna neno fulani halifai, kura ya maoni tayari kubadilisha yale masilahi

Bwana Nyawa anauliza kuna wale ambao wanapewa tenders halafu wanafanya kazi halafu haziishi, jibu lake ni rahisi sana, sasa hiyo ni kazi ya Serikali ya Wilaya. Hiyo ndiyo inaangalia, inatengeneza barabara, maji misitu, ma-hoteli, hiyo ni kazi yao, hao ndio wana tender sasa ndio wanatoa. Wakishindwa ni wao wenyewe, lakini tumeaandika pale hiyo ni kazi yao.

Kuna matatizo ya kazi, na uchumi umezorota. Principle yetu tumeandika hapa tunataka good governance na economic prosperity, principle yetu, broad principles. Kila anaye fanya kazi ya taifa hili ajue kwamba lenga haya maswala mawili. Prosperity na good governance. Sasa haya mambo mawili yakiwweko ndiyo kazi zinakuja. Good governance ni kwamba hakuna corruption. Watu wengi wamekosa kazi, kwa sababu ya corruption, usifikiri kwamba ahakuna kazi hapa Kenya, kazi zipo. Lakini sasa ikiwa tumeletewa kiwanda cha billion mbili kitengenezwe tutolewe kaz 50 halafu zile pesa ziliwe, zile kazi wafikiri zitapatikana?

**Chorus:** Hazipatikani.

**Com. Swazuri:** Ikiwa kumetolewa billion 5 tujengewe viwanda sita Kenya nzima zipatikane kazi ya elfu hamsini, billion tano, zimeliwa billion 4, zitapatikana kazi hapo? Lakini je tukifunga ile madirisha, tukisema ukiletwa pesa lazima lifike kwa Bunge la Jimbo, Lazima ziende kwa Bunge la chini la Wilaya, Bunge la Location, ndio waamue project hio na ile, watakuwa na uhalifu hapo. Sasa kama nimekuja mpaka Location wa Kinango nimepatiwa, kiwanda kimejengwa, kwa nini kusipatikane kazi? Na mwenye kuajiri ni District Government, kwa hivyo sasa tuko tayari, ukosefu wa kazi tukijaliwa tumeuondoa kabisa. Na Serikali hizi za Majimbo na za Wilaya zimepewa kazi ya kufanya physical planning, economic planning, hawa wenyewe waseme---development planning. Miaka mitano ujao tunataka tuwe na barabara fulani, hawa wenyewe hakuna kungojea.

Hilo swali nimejibu hata swalala la uchumi kwamba uko chini Kinango, na kilimo, na mikopo haipatikani, sasa mambo yote haya sasa yamesawazishwa Jimbo litaamua, Wilaya itaamua, ndiyo iko uwezo. Kama mikopo imetoka mahali fulani haitolewi sasa mpka iingie kwa Serikali zile, zijadili zisambaze. Watu wamelalamika kwamba kuna pesa huja ofisini, tunasikia kunapesa kimekuja lakini hatushiki. Vikundi vya akina mama wameletewa pesa lakini hazifiki kule chine, malalamiko hayo tumeyapata wakati wa kusikiza maoni. Sasa itakuwa ni lazima kwanza ikifika Serikali ya kama ni Location, ya District, ya Jimbo ndiyo itaamua kwamba tumepata millioni tano ilikuwa ni za nani? Akina mama, haya akina mama, kundi la akina mama.

Na wasipofanya vile, automatically hiyo ni kazi moja wamekiuka, sign zinakuja nje. Umuhimu wa hio kazi hiyo ni kwamba mtahusika sana sasa kujadili mambo ile. Nimesema Katiba hii imetoa nguvu kwa wananchi wahusike. Wakati wowote nyinyi mtaitwa, na kura zitakuwa mara nyingi kura zitakuwa kila siku, mkutano ni kila saa, mulize je hizi sawa au vipi, kila saa Electoral Commission kazi yake ni kufanya Civic eduction itakuja saa yote, jamani tuwataka twaaeleze maana ya governors, nini msichoke, mapaka watu watazoea kwamba hii ni nchi yetu. Kiongozi atakuwa si wenyewe ndiyo kwamba anakuta hawa ataniambia nini, a a, kiongozi ikiwa Katiba itafuwata, kiongozi sasa atakuwa anawanyenyekea sasa, jamani kwani mwasema aje? Jamani kwani ni vipi, manaake bila hivyo, out, atatolewa tu. Hii ndiyo msingi ambao tumeifanya tunataka kubadilisha ile sura ya kwamba sheria zote zinatoka juu, zinakuja chini, sasa tunataka nguvu zitoke chini sasa ziende juu. Wananchi wakisema wanataka hivi, Serikali ya Kijiji itazungjumza ipelekee Serikali ya Location izungumze, watakaokubaliana itekelezwe hapo hapo. Likishinda Serikali ile ya juu, hivyo mpaka Serikali ya Jimbo, ikishaundwa ndio tutapeleka Nairobi. Haya watu wengine kumi. Nitawapatia preference ambao hawajasema mwingine, Bwana delegate pale. Kwanza tuna wale wakikilishi wawili wa Kwale wawili tayari tukonao. Tulisema kwamba tutachagua watu watatu. Kila Wilaya itachagua watu wa tatu kwenda kwenye Kongamano la Kitaifa. Ambao wataungana Wabunge, wataungana na vyama vya kisiasa, watu karibu mia saba. Wawili tukonao, huyo ni mwakilishi wa Kwale District lakini ametoka Kinango Constitutiecy. Walifanya uchaguzi Kwale, walichaguliwa kwenya uchaguzi Kwale tarehe kumi na saba. Na huyu Bibi hapa naitwa Fatuma Boi, ametoka Msambweni Constitutency, anawakilisha Wilaya ya Kwale. Wa tatu hayuko hapa, Ni Bwana Ali Mwakwere, mtu wa Golini pale, mtoto wa Mzee Waraka. Huyo ndio wakilishi wa Kwale District, anarepresent Matuga Constitutuency. Hayuko. Fatuma ndiyo huyu, hawa ndio watu ambao majukumu ya kwenda kupigania haya mnayosema tumewapatia hao. Sasa jana niliwambia vizuri sana,

Kwale kimekinyimwa haki zake lawama ni kwenu. Ubaya ni kwamba hatuna njia ya kuwatoa. Haya wa kwanza, wa pili, wa tatu, Reverend uko na pendekezo, haya anza wewe.

**Edward Hali:** Kwa majina ninaitwa Edward Hali, mimi ni Mwana Kamati kwa hii Katiba. Kuna swalallingine ambalo sikulisikia katika wakati huu ambao tulikuwa nao, na kuhusu mahospitali, yaani matibabu. Hilo sijui kama ulilisoma huko ndani pengine nilikuwa nimeaandikwa ama namna gani, ningetaka lifafanuliwe ili tusikie. Na kama halitafafanuliwa ama litafafanuliwa kuwa hakuna si free, tupate pia tupewe viwango kiwango vingine ambavyo tunaweza kuchangia kuwa kuna maradhi mengine ambao ni kama malaria. Maradhi ya malaria kwa kweli, tunasema ukimwi unamaliza, lakini kunao maliza sana ni malaria, ambao hiyo malaria unaweza kuwekwa limit yake ya kuwa sasa hiyo iwe itakuwa kama hivi juzi kulikuwa na mkasa mwingine huko bara ikawa malaria inatibiwa free. Kwa hivyo hiyo utatufafanulia vizuri.

Swala lingine ambalo nilikuwa nataka kutilia katika Katiba hii yetu ni kwamba mimi si mzee sana, lakini kisoma changu nilisoma kizamani kidogo. Na ningependelea, kulinganan na hii Katiba yetu mpya ambao tukonayo, irudishe somo lile ambalo wengine wetu hapa tulisoma lilikuwa linaitwa Civic Education, Civics. Hilo swala hjilo kulingana na hii Katiba kama somo hilo itakuwa itakufundishwa shule kutoka class cha tatu mpaka class cha nane, hii Katiba itakuwa sasa inakuwa na wenyewe ambao wanakuwa nayo. Swala lingine nafkiri tulizungumza kuhusu mahali ambapo kutakuwa na korti ambalo tunaweza kushitaki katika kutetea haki zetu. Hizi korti hizi tafadhali tungeomba ziwe karibu na wananchi. Kwa hayo machache, asanteni.

**Raphael Ndeme:** Kwa majina mimi ni Raphael Bombo Wandame ni Mwakilishi wa Kwale District katika lile Kongomano wa Taifa. Na mimi ninajua hii District yetu vizuri sana. Ningetaka kuzungumza kuhusu uchaguzi wa hii Serikali wa Wilaya. Tunajua kwamba sehemu zetu nyingine ni kavu, watu wengi hutoroka huko, kwenda kutafuta mashamba kwingine, na ukiangalia population kama Kinango Division, waweza kuilinganisha na population ya Ukunda Location. Sasa, kama uchaguzi itakuwa ni kila mmoja afanye compaign kwa District nzima mimi naona kuna owezekano Wajumbe, wale ambao watakwenda kwa Serikali ya Wilaya kutoka sehemu moja. Kutakuwa hakuna usawa. Ombi langu ni kwamba ikiwezekana kuwe na mipango kwamba either kila division ama kila constituency ichague watu wake fulani wapelekwe kule. Asante.

**Rev. John Katana:** Mimi ni Rev. Katana. Nilikuwa na maswali mawili moja limejibiwa lakini sikutosheka, nataka nifafanuliwe kidogo. Ya kwanza ni kuhusiana na elimu. Tumeelezewa kuhusiana na kuanzia nursery mpaka class 8 kwamba ni bure, lakini hiyo ni part A. Part B ambayo tulizungumza na sikuisikia ni kwamba tulisema elimu ni ya bure. Na ni ya lazima, je swali ni kwamba, kunao wazazi wengine sehemu nyingine, watoto wapo, lakini hawataki kuwapeleka shule. Si mvulana ama si msichana. Sasa basi kwa sababu elimu ni ya lazima na lazima mtoto ana haki ya kusoma kama hivyo ambavyo tumesomewa haki za watoto. Je huyu mzazi ambaye hataki kupeleka mtoto wake shule afanywe je?

Swali la pili ni kwamba level ya government tumesema kwamba kuna Vilage, Location District na Province. Tumesikia tu jina la kiongozi wa District, tukaambiwa ni governor. Je Kufikia kwa Villlage, Je yule kiongozi, atakuwa anaitwa jina gani, na tukifika

kwa Location ataitwa jina gani, na tukifika kwa Province ataitwa jina gani?  Asanteni.

**Com. Swazuri:** Haya, upande wa matibabu, Bwana Edward, unasema kwamba matibabu ni lazima yapatikane kwa Mkenya yoyote, lakini tukiangalia Section 57 tumeelezwa matibabu ni lazima yapatikane kwanza kwa emergency treatment, kama upepigwa dafrau hivi upelekwe hospitali, kwani ni lazima upatiwe, sio kwamba ulizwe utoe pesa ndiyo upatiwe, emergency treatment ni lazima.  Lakini tumesema schedule 7 ukiangalia number 5 imeeleza kwamba Serikali ya Wilaya, ni lazima ihudmie na kutoa huduma zinazo fuata:  ehlimu, hosipitali, na kadhalika.  Sasa imekuwa ni kazi ya nani? Serikali ya Wilaya.  Hio ni Serikali ya Wilaya tumesema ndio itakuwa na jukumu hilo.  Sasa itapanga kama itacharge kiasi gani na kiasi gani lakini principle yetu ni kwamba iwe ni ile ambao inatosheana na wananchi, affordable. Kama watakuwa na wa hizo resources waseme wanatoa matibabu bure kabisa, pia wana uhuru wa kutoa hiyo. Tumeweka open kabisa.  Kwa hio vile mnarudi kufanya kazi zaidi, ndiyo mambo yenu yanakuwa rahisi zaidi.

Civics, ni kweli watu wengi wali sema hivyo, na tutaenda kuiangalia, tunataka tulifikiria kwamba tukiwapatia Electoral Commssion watakuwana pamoja na hawa wana siasa, viama vya kisiasa, itakuwa ni bora lakini tutaangalia mpango wa kuirudisha; iwe ne somo ni lazima.  Kama ambavyo tullikuwa tukisoma zamani civics. Lakini tukisema hivyo lazima tukase kamaba pahali pengine, ndio maana tumesema kwamba viongozi watateuliwa na Bunge na watateuliwa kwa misingi fulani. Zamani ulikuwa ukisikia kama ni Secretary, unaweza kwanza standard 1 mpaka standard 7, Permanent Secretary ni huyo huyo mmoja, au sivyo.  Alikuwa ni Permanent kweli.  Lakini siku hisi hata niki kuuliza ni nani huwezi kumjua.  Wanabadilishwa siku mbili baadaye kwa sababu ya uchaguzi wao unategemea ofisi fulani.   Hata Mawaziri saa hizi mimi pia nime iacha ya kuhesabu au kujua ni nani, maanake ikimaliza miaka miwili mara yule abaadili—mara hivi tu sasa hata kama utafundisha hiyo civics, hawa watoto tutawafundisha nini?  Mambo yana badilika kilasiku.  Lakini sasa tumekaza hapo. Tumesma, ukuchaguliwa vile inajulikana, msimamo ni ule ule.  Sasa ukienda kuwafundisha watoto, Waziri wa maji ni nani? Wanajua automatically ni fulani.

Courts near the people, tumesema mahaka lazima kweli ziwe karibu na wananchi na tumesema legislation should be encated to ensure couorts zinakuja karibu.  Kurahisisha hiyo tufanye iwe haraka pia tuimesema traditional courts zitaanza chini kabisa kabla kuenda kwa hizi mahakama za Serikali.

Bwana Raphael pale ameeleza kwamba ikiwa Wilaya hazitaangalia pengine wale Wajumbe wote watatoka sehemu moja ni kweli, kwa hivyo tutaenda tukaangalie kama tunaweza kuzi-limit kwamba kila constituency au kila Location iwe na mtu mmoja au wawili, maanake ile number ni kama 30, tutaangalia labda tuzigawaye kwa kila disíon au kwa kila constituency ili watu wasioneane.

Elimu section 58, nimesahau kusema tu pale lakini elimu ni ya bure na ni ya lazima.  Si bure hivyo hivyo, elimu ni ya bure tena ni lazima, na sheria zitaundwa kwa hakisha kwamba wazazi ambao hawafuati sheria hio watakuwa matuba Katiba kwanza halafu

pili hadhabu yao ikaandikwa. Kwa hivyo wazee wangu wengi mwajua hapa huwa tunatilia ili swala ili tunaliweka nyuma sana. Mimi ninajua kwetu ni bhuku huku, unajua watoto wengi wengi wakisoma Mungu mwenyewe ndiye amewasaidia. Lakini wazazi, najua kuna wazazi hata mimi kwangu kijijini anafanya kusikia kwamba mtoto wake amemaliza. Wampelekea majibu mzee—Ah, hata wewe ulifanya. Mzazi huyo. Mtoto wa standard 8 amemaliza ndio mzazi yuashtuka kwamba alah hata wangu amefanya. Sasa asipoenda pia yeye hua hajui. Lakini sasa ni lazima. Wazee elimu ni bure, lakin inalazimishwa, kama vile zamani kuwa si rahisi kuona watoto wanakaa bure. Halafu Villlage Council, hii haina yule kinara, anayepatikana jina la government, hawa watachagua wenyewe lakini yule kinara wa Villlage, saa hizi ni Villlage Chairman, hakuna jina lile tumempatia pale hiyo tutakwenda kuiangalia.

Halafu ile Location anaitwa Locational Adminstrator. Kulingana na hapa tumemuita Locational Adminstrator, halafu kwa District, hapa tumeandika District Administrator, alakini tumetukitumia majina tofauti tofauti. Saa nyingine tunaita District Governor. Wengine walipendelea hivyo, wengie wakasema aitwe District Adminstrator. Na jina hilo pia ikaenda kwa Provincial, tunamuita either Provincial Adminstrator, au tumemuita Provincial Governor. Hapa tumeandika Provincial Adminstrator. Wengine pai wakasema tumuite Senator huyo wa District, lakini tumekubaliana na jina hilo la Provincial Govenor or Provincial Adminstrator. Officially itakuwa Adminstrator lakini the two of them mean the same. Haya nafikiri tume maliza.

Sasa baada ya hapa District Cordinator Bwana Mweru anatakikana kisheria kufanya mikao zaidi na wnanachi wa Kinango. Kama atakwenda Samburu, atakwenda Zurungani, kama atakwenda Ndavaya, ni lazima afanye mikutano kama hii, ambapo wananchi watatoa hoja zao kuhusiana na huu mswada huu. Halafu yeye atatuletea haya mambo maanake kuna wengi hawakufika hapa kwa sababu wako mbali. Lakini yeye ni mwepesi wa kufika kule tumempatia sheria hiyo, jukumu hilo, aende akakutana na wananchi, halafu pia yale maswali atatupia sisi, halafu tutapeleka kwa Kongamano la kitaifa. Kwa hivyo huu ni mwanzo hapa. Leo lakini ukisikia uko ndani ndani, chini chini bado kuna mikutano kama hii lengo ni lile lile, tu hakikishe kwamba mpakak kila mtu ame ridhika kwamba bwana sasa mambo yangu yako sawa. Tusije tuka fanya halafu baada ya siku mbili tunataka kurekebisha Katiba. Baada ya mwamka moja, hapana, tunanataka kurekebisha Katiba, hapa.

Kutakuwa na mikutano baada ya hapa, yeye na Kamati wale Committtee Members wake. Sheria tumewaambia ni lazima muwafanyie mikutano hawa wananchi zaidi ya hii. Wale ambao hawakuweza kufika, ni lazima mpange kila Location au kila division, muweke nyinyi wenyewe mikutano wnananchi waweze kuchangia zaidi. Nafikiri tutakomea hapo, ninawashukuru sana kwa kufika, kuna mzee ana swali hapa?

**Mzee (Name unannounced**) Tulizungumza kusema hawa watu wa County Council ambao wanaitwa ni wa County Council (in kikamba) hawa watu ambao ni Madiwani, hawa watu tulizungumza habari yao kwamba wale hatuwaoni kwamba wanakazi yoyote. Wanangojea pesa za Serikali kula, lakini sikusikia majibu kama wako au hawako.

**Tobi Keya:** Mimi ninatitwa Tobi Keya. Shukrani kwa Commission kwa sababu yale mambo ambayo tulizungumza,

mumefanyia kama vile ambavyo tulizungumza. Nataka kusema ya kuwa wale ambao wana payuka huko kando kando ya kuwa Commission imefanya mambo yao kando kabisa, wajue sisi tunakataa, na tuko tayari vyovyote vile kusimama na hii Katiba. Halafu nilikuwa nasema hivi pia, mume sukuma karibu kilakitu katika hizi Local Government, ya kuwa mambo ya employment, mambo ya education, kila kitu inafanywa na Serikali za mtaa. Lakini sasa kitu ni kuwa kwa mfano huku unaona, rasilmali nyingi sana huku zimechukuliwa, zikasukumwa huko kwengine kutengeneza ma hospitali, universities, nini na nini na nini, huku kwetu hakuna chochote. Sasa kama kila kitu kitaletwa huku na huku hakuna chochote, kuna mpango gani ya kama vile ambayo vimepelekwa kule hata kama vina weza nyakuliwa ki vyovyote vile vikaja huku kukawa ne usawa halafu ndiyo watu watasongea mbele?

(**Name unannounced)** Asante sana, kupewa hii fursa. Swali langu la nyongeza katika Katiba yetu au vile mazungmgmuzo vilivyoanza mpaka hapa tumefikia, kuna kitu moja kimeniijia wakati huu, hasa kuhusiana na vijana. Sikusikia ikizungumziwa kikamilifu. Vijana watatumikia taifa hili ki vipi, na kwa njia gani watapata uwezesho katika maendeleo ya taifa kwa jumla?

**Ruwa Ngundo**: Mimi naitwa Ruwa ngundo kutoka Magulani. Swali langu ni kwamba hii sheira inarekebishwa, na kuna wafungwa---sheria imerekebishwa mpya, na mtawala atakuja mpya je wafungwa nao watatolewa, ama watakaliwa na ile sheria ya zamani? Pili, silaha ya mwananchi ni kura kumchagua anayempenda. Kura zilichukuliwa. Kuna wengine walikuwa hawajapata vitambulisho na wamefika umri wa kuchukua vitambulisho, je kutatokea nafasi wapate vitambulisho wale au ni basi, ni hayo tu?

**Com. Swazuri:** Kuna wengine wamekuja kuchelewa, nafikiri. Tumesema kwamba nominated Councillor, hata hatukuwataja manake hawamo, wananchi watachagua wenyewe moja kwa moja wale watu watu 30 ambao wataunda Bunge la Wilaya, kwa hivyo hakuna nominated Councilor, hakuna kabisa. Halafu, rasilmali ambazo zimechukuliwa huku zikapelekwa huko. Kwanza tunataka kusema kwamba sababu ya kuleta Serikali za Majimbo na za Wilaya ni kwamba wananchi wasifikirie ni masikini. Wanatakikana rasilmali walizo nazo hapa nyumbani wazitumie vile ambavyo zinaweza kuwafaidi. Okay, halafu tumesema Serikali ya Central iko na uwezo zaidi wa kugawanya rasilmali za kitaifa. Kuna national resources, kuna Provincial resources, kuna disteict resources, kuna District resources, kuna Locational resources. Serikali inahaki ya kuchukua hapo hapo halafu kugawanay hata kule ambapo hakuna. Hio tumeandika pia.

Halafu vijana, tumesema hatutaki kubagua wananchi wa Kenya. Huo ni msingi wetu tumeutoa. Wananchi wa Kenya hatutaki kuwabagua kwa umri, kwa jinsia, kwa eneo ka kabila kwa dini kwa rangi, kila mwananchi wa Kenya ana haki yake. Kama ni vijana wanajisikia wanan taka kufanya uongozi, tumewapatia, miaka 21 unagombea uchaguzi. Kwa hivyo haki zote za kila mtu ziko, hata wale wasiojiweza tumesema tuwapatie haki zao. Hatukuweka kwamba vijana, au hivi na ah ah! kila mtu. Lakini tume sistiza zile haki za wale watu ambao wananyimwa, ndio maana tume ziandika. Hatukuandika haki za wanaume mumeziona? Kwa sababu hawa mambo yao yanajulikana tayari. Lakini haki za akina mama ambao wana nyimwa nyimwa, tume yata. Haki za Wazee ambao hasa ni mapengo hawa waende zao, tumeziandika. Haki za wale vile mumeambaia hapa na huhu ana tabu

gani, sasa tumeziandika.

Wafungwa, Katiba sheria ni mpya, lakini kama amefungwa miaka kumi, sasa huyo bado ana miaka yake kumi, ata serve. Tunasema wafungwa kuanzia ile Katiba itakayoanzishwa. Wafungwa wote walioko ndani hawatatolewa kwa sababu Katiba imekuja mpya, lakini mambo yao yatabadilika vile hali zao za kuishi kule zitabadilika kulingana sheria mpya. Ikiwa hawana nguo hivi sasa, sheria hii ikipitishwa lazima wapatiwe nguo mpya. Ikiwa hawana vitanda sheria hii ikipitishwa ni lazima. Ikiwa hakuna vyoo, sheria hii ikipitishwa ni lazima. Sasa alifungwa, aka fungwa muwaka ujao hiyo ni lazima.

Kura tumesema sasa, sijui waeleza kwa sasa ama kwa hapo tujapo lakini ikiwa ni sasa, kura zishaandikishwa, nafikiri walifunga register ya kura. Hata wale ambao wanataka kwenda kuona kama majina yao yako ama hayako, walipewa muda wasiku 60 kulingana na sheria, sijui kama umeisha au bado kwenda kuangalia register kama majina yao yako, unaweza kulamanika kwamba kwa nini mimi ni kadi ya kura ninayo lakini majina yangu hayako. Hilo lipo, lakini tumesema kwamba kitambulisho ni lazima kupata kitambulisho hivi sasa, bado kuna ruhusa. Lakini tu Katiba hii ikipitishwa, tumesema kwamba kitambulisho kwanza ni lazima, birth certificate ni lazima, passport mtu akitaka ni lazima. Passport itatolewa kwa mwananchi yeyote yule haya, chukueni. Kuna wengi hawataki kusasfiri nje hya nchi. Lakini anaye taka yeye lazima atapewa. Halafu tukasema kwamba akisha pata kitambulisho mwananchi yule anaandikisha kura siku zoyote anayotaka. Continuous voter registration. Miaka mitano yeye yuandikisha kama haja pata nafasi ana nafasi ya kuandikisha. Hiyo ndivyo ambavyo tunaomba. Kwa hivyo sasa nitaita mzee moja wa Kiislamu atufungie kwa maombi. Tumeanza wa wa Mkristo tumalize na Muislamu. Waislamu hakuna Bwana Saidi Mwachiti mnamuona kama--- tupatia dua Bwana.

**Prayers**: **Saidi Chti Mwachiti**: (Islamic prayer in arabic) Kwa jina ninaitwa Saidi Chiti Mwachiti.

Meeting ended at 1.00 p.m.

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**